JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA WAZIRI MKUU

TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

HALMASHAURI YA WILAYA MISSENYI

MPANGO MKAKATI WA MIAKA 5 (2014 – 2018)

OFISI YA MKURUGENZI MTENDAJI
HALMASHAURI YA WILAYA MISSENYI
Simu: 0732-983531
Faksi: 0732-983307
Barua Pepe:missenyicouncil@yahoo.com

Januari, 2015

MPANGO MKAKATI WA HALMASHAURI 2014 - 2018

YALIYOMO

Vifupisho vya maneno..... i
Maelezo ya utangulizi ya Mhe. Mwenyekiti wa Halmashauri ii
Maelezo ya utangulizi ya Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri---------- iiii

SURA YA I
Utangulizi.....

SURA YA II
Uchambuzi kwa kila Sekta/Kitengo----------

SURA YA III
Dira, Dhima, Madhumuni na Amali (Core Value) na maeneo yenye matokeo muhimu....

SURA YA IV
Malengo na utekelezaji wa Mpango Mkakati kwa miaka 5 ijayo ----------

SURA YA V
Mpango kazi wa kutekeleza Mpango Makakati Ufuatiliaji na Tathmini ----------

SURA YA VI
Ufuatiliaji na tathmnin ----------

Vifupisho vya maneno

CBOs – Community Based Organizations
CSOs - Civil Society Organizations
CUF - Civil United Front
CHADEMA- Chama cha Demokrasia na Maendeleo
DALDO - District Agriculture and Livestock Development Officer
DCDO - District Community Development Officer
DCO - District Cooperative Officer
DE - District Engineer
DED - District Executive Director
DEO (M) - District Education Officer (Primary)
DEO (S) - District Education Officer (Secondary)
DFsO -District Fisheries Officer
DIA - District Internal Auditor
DLaDO - District Land Development Officer
DMO - District Medical Officer
DNRO - District Natural Resources Officer
DPLO - District Planning Officer
DT - District Treasurer
DVO - District Veterinary Officer
DWE - District Water Engineer
FsO - Fisheries Officer
HBF - Health Basket Fund
HIV/AIDS - Human Immune deficiency Virus/Acquired Immune Deficiency Syndrome
IEC - Information Education Communication
LAAC - Local Authority Accounts Committee
LGAs - Local Government Authorities
LGCDG - Local Government Capital Development Grant
LO - Legal Officer
MKURABITA – Mpango wa Kurasimisha Biashara za Wanyonge Tanzania
MM - Mpango Mkakati
MTEF - Medium Term Expenditure Framework
NAO - National Audit Office
NEC - National Electral Commission
NGOs - Non Governmental Organizations
PMO-RALG- Prime Minister's Regional Administration and Local Government
PMU - Procurement Management Unit
PPA - Public Procurement Act
PPR - Public Procurement Regulation
SACCO - Saving and Credit Cooperative Societies
TACAIDS - Tanzania Commission for AIDS
TANROADs -Tanzania Roads Agency
TLP – Tanzania Labour Party
TTCL - Tanzania Telecommunication Coperation Limited
TASAF III - Tanzania Social Action Fund III
VVU/UKIMWI – Virusi vya UKIMWI/ Ukosefu wa Kinga Mwilini
VEOs - Village Executive Officers
WDC - Ward Development Committee

Maelezo ya utangulizi ya Mhe. Mwenyekiti wa Halmashauri

Mpango Mkakati wa miaka 5 (2014 – 2018) unalenga kutimiza Dira na Dhima ya Halmashauri kwa: Kutoa huduma bora ya kijamii na kiuchumi kwa Wananchi wake na hatimaye kujenga uchumi imara na kuwa maendeleo endelevu ya Wilaya

Mpango unasisitiza kuongeza tija kwenye uzalishaji wa mazao ya: Kilimo, Mifugo na Uvuvi kwa kuimarisha huduma za ugani, miundo mbinu, kuweka na kukopa (SACCOS) pamoja na kuhimiza Vikundi vya kiuchumi vya Wanawake na Vijana.

Maeneo yaliyopewa kipaumbele wakati wa kutekeleza Mpango huu ni pamoja na: Kusimamia na kuongeza mapato ya ndani ya Halmashauri, Kusimamia sheria za Fedha za Serikali za Mitaa, Kusimamia na kuendeleza Rasilimali watu ili wafanye kazi kwa tija na kutoa huduma bora, kuwalinda Raia na mali zao kwa misingi ya Utawala bora.

Aidha, Halmashauri ya Wilaya Missenyi imeweka mkazo katika kuishirikisha jamii na Asasi mbali mbali kutekeleza masuala Mtambuka (Mazingira, UKIMWI/VVU, Rushwa, Utawala bora na Kuwawezesha Wananchi kiuchumi).

Mpango pia unaweka bayana mambo ya msingi yanayowezesha utekelezaji wake, hasa; Uchambuzi wa hali halisi, Dira na Dhima, Madhumuni, Malengo na Mikakati mahsusi ya Wilaya.

Muhtasari wa Viashiria vitakavyopima mafanikio ya utekelezaji pamoja na takwimu zinazoonesha hali halisi ya utoaji huduma kwa sasa nazo zimewekwa kwenye Mpango Mkakati huu.

Napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa wale wote walioshiriki kwa njia moja au nyingine kwenye mchakato huu wa kuandaa Mpango Mkakati wa Halmashauri wa miaka 5 (2014 – 2018). Shukrani maalum ziwaendee Waheshimiwa Madiwani wote, Wakuu wa Idara na Vitengo, Wawakilishi wa Asasi za Kiraia, NGOs, Asasi za Kidini, Taasisi za Serikali Viongozi wa Vyama kwa ushiriki wao makini mwanzo hadi mwisho wa mchakato.

Mwisho lakini si kwa umuhimu, natoa shukrani za kipekee kwa ndugu Jommo Watae 9Afisa Mipango wa Wilaya) kwa juhudi zake za makusudi za kuwezesha mchakato wote wa kuandaa Mpango Mkakati wa Halmashauri wa miaka 5 (2014 – 2018). Ni matumaini yangu kuwa Mpango huu ukitekelezwa kwa kuwashirikisha Wadau wote wa Maendeleo, Wilaya itapiga hatua kubwa ya maendeleo kwa miaka 5 ijayo.

Mhe. William F. Katunzi
Mwenyekiti wa
Halmashauri

Maelezo ya utangulizi ya Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri

Mpango Mkakati wa Halmashauri ya Wilaya Missenyi ni wa miaka 5 (2014 – 2018) ulioandaliwa kwa kuwashirikisha Wadau na kuongozwa na mambo muhimu yafuatayo: Sera za Kitaifa na za Kisekta, Malengo ya Maendeleo ya Mileniam, Dira Maendeleo ya Taifa 2025, MKUKUTA III, Dira na Dhima ya Halmashauri, ambazo zinasema;
Dira: "Kuwa na Wananchi wenye maendeleo endelevu na miundo mbinu na huduma za kiuchumi na kijamii iliyo bora ifikapo 2025"

Dhima: "Kuijengea uwezo Jamii na taasisi zake ili kutoa huduma bora za kiuchumi na kijamii kwa kushirikiana na Wadau kwa kuzingatia Utawala Bora".

Wakati wa kuandaa Mpango Mkakati huu, vipaumbele na mahitaji halisi ya Wananchi wa Missenyi na Mkoa kwa jumla vimezingatiwa. Aidha, Madhumuni, Malengo na Amali za Msingi za Halmashauri pia zimezingatiwa.
Wadau mbali mbali wameshirikishwa kwenye mchakato wote wa kuandaa Mpango Mkakati huu
Mpango Mkakati wa Halmashauri una sura 6, ambapo sura ya I ni Utangulizi pamoja na sura ya Wilaya. Sura ya II ni Uchambuzi wa kila Sekta na Kitengo. Sura ya III ni Dira, Dhima, Amali na maeneo muhimu yenye matokeo muhimu.

Sura ya IV ni maelezo ya kina kuhusu Malengo na utekelezaji wa Mpango Mkakati kwa miaka 5 ijayo. Sura ya tano inaelezea Mpango kazi wa kutekeleza MM na Sura ya VI ni Ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa MM

Kwa kuhitimisha, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Watumishi wa Halmashauri ya Wilaya ya Missenyi na Wadau wote walioshiriki kwenye mchakato wote wa kuandaa Mpango Mkakati wa miaka 5 (2014 – 2018).

Ni matumaini yangu kuwa; Halmashauri kwa kuwashirikisha Wadau wote itatekeleza Mpango Mkakati huu kwa ufanisi mkubwa kwa nia ya kutoa huduma bora kwa Wananchi na hatimaye kuboresha hali ya maisha ya Wananchi wote kwa kuzingatia Utawala Bora.

Elizabeth S. Kitundu
Mkurugenzi Mtendaji
Halmashauri

SURA YA I

1.0 Utangulizi

Uandaaji wa Mpango Mkakati wa miaka 5 (2014 – 2018) wa Halmashauri ya Wilaya Missenyi umezingatia misingi ya Majukumu ya kisheria ndani ya mipaka yake, ambayo ni; kutoa huduma bora kwa Wananchi wake kwa kuwashirikisha Wananchi wenyewe na Wadau wa maendeleo walliomo ndani na nje ya Wilaya

Dira, Dhima, Madhumuni, Malengo, Amali na Mikakati mbali mbali imewekwa kwa utekelezaji ili kuhakikisha ufanisi na tija katika kuleta mafanikio wakati wa utekelezaji

1.1 Mchakato wa kuandaa Mpango Mkakati

Kwa mujibu wa sheria ya Serikali ya Mitaa namba 9 ya mwaka 1982, Kila Halmashauri inatakiwa kuwa na Mpango Mkakati utakaotumika kwa miaka 5 kama Mwongozo unaoelekeza mambo muhimu na vipaumbele vinavyotakiwa kuwemo kwenye Kitabu (MTEF) cha Mpango na Bajeti ya Halmashauri kila mwaka.

Watumishi wa Halmashauri na Wadau mbali mbali wameshirikishwa kwenye mchakato wote wa kuandaa Mpango Mkakati, huku rasimu yake ikipitishwa kwenye Vikao vya kisheria vya Halmashauri, vikiwemo: Timu ya Menejimenti ya Halmashauri, Fedha, Uongozi na Mipango na Baraza la Madiwani

1.2 Malengo ya Mpango Mkakati

Mpango Mkakati wa miaka 5 kama mwongozo wa utoaji wa huduma bora kwa Wananchi, una malengo makuu yafuatayo:

- Kuboresha utekelezaji kwenye Halmashauri
- Kuzishirikisha Sekta zote, Jamii, Wadau na kutumia rasilimali zilizopo ndani na nje ya Wilayani pamoja na mbinu mbali kwa nia ya kuleta maendeleo.
- Kuhakikisha vipaumbele vya Jamii vinashughulikiwa kikamilifu kwa kutumia nguvu za pamoja
- Kuwa na mtazamo wa pamoja katika kutekeleza vipaumbele vya Jamii na kuwa na utaratibu mzuri wa kufuatilia, kusimamia na kutathmini utekelezaji wa miradi iliyopangwa

1.3.0 Taarifa muhimu na sura ya Halmashauri ya Wilaya Missenyi

1.3.1 Jiografia ya Missenyi na mipaka yake

Halmashauri ya Wilaya Missenyi ilianzishwa mwaka 2007 baada ya kugawa Halmashauri ya Wilaya Bukoba, na ni miongoni mwa Halmashauri 8 za Mkoa wa Kagera. Halmashauri zingine ni: Biharamulo, Bukoba, Bukoba Manispaa, Karagwe, Kyerwa, Muleba na Ngara.

Halmashauri ya Wilaya Missenyi iko upande wa Kaskazini Magharibi mwa Mji wa Bukoba na imepakana na Ziwa Victoria kwa upande wa Mashariki, Halmashauri ya Bukoba kwa upande wa Kusini, Halmashauri ya Kyerwa kwa upande wa Magharibi na Nchi ya Uganda kwa upande wa Kaskazini.

1.3.2 Eneo la Wilaya

Wilaya ya Missenyi ina jumla ya eneo lipatalo hekta 270,876, na kati ya hekta hizo, jumla ya hekta 99,726 zinafaa kwa kilimo na hekta 63,884 ni kwa ajili ya malisho ya mifugo. Kwa sasa eneo linalotumika kwa kilimo ni hekta 59,840 na hekta 31,547 ni maeneo ya misitu ya hifadhi, sehemu kubwa ikiwa ni Hifadhi ya Misitu ya: Minziro, Mnene, Kikuru, Lwasina, Kantare, Kikongoro, Ruchwezi na Bushenya.

1.3.3 Muundo wa Utawala

Wilaya ya Missenyi imegawanyika katika Tarafa 2 za: Missenyi na Kiziba, Kata 20, Vijiji vilivyosajiliwa 77 na Vitongoji 355

Mhe. Mbunge ni mmoja wa Jimbo la Nkenge na Wahe. Madiwani wako 27 (20 wa kuchaguliwa na 7 ni wa Viti maalum).

Vyama 5 vinavyojishughulisha na masuala ya Siasa Wilayani Missenyi ni: Chama Cha Mapinduzi (CCM) – ina asilimia 83.9 ya Viongozi wa Serikali za Mitaa, CHADEMA ina asilimia 15.6, CUF asilimia 0.18, NCCR – Mageuzi asilimia 0.25 na TLP asilimia 0.07

1.3.4 Idadi ya watu

Kwa mujibu wa Sensa ya watu na makazi ya mwaka 2012, Wilaya ya Missenyi ina watu 202,632 (Wanawake ni 102,547 na Wanaume ni 100,085) na Kaya 35,699. . .

1.3.5 Hali ya Hewa

Wilaya ya Missenyi ina Kanda mbili za mvua: Tarafa ya Missenyi inayopata mvua nyingi (mm 1,400 – 2,000) na Tarafa ya Kiziba inayopata mvua ya wastani (mm 600 – 1,000). Wilaya ina wastani wa nyuzi joto kati ya 15^{o}C na 28^{o}C.

1.3.6 Ulinzi na Usalama

Pamoja na Wilaya kupakana na Nchi jirani ya Uganda, hakuna matukio makubwa yanayovunja amani na kuhatarisha usalama wa Raia na mali zao mpakani.

Aidha, Kamati za ulinzi na usalama za Vijiji zinatekeleza majukumu yao ipasavyo na Wananchi wanashiriki kikamilifu katika shughuli zao za maendeleo bila kikwazo cho chote

1.3.7.0 Shughuli za kiuchumi

Takribani asilimia 90 ya Wakazi wa Halmashauri ya Missenyi hujishughulisha na Kilimo na Ufugaji, asilimia 5 ni Wavuvi na asilimia 5 ni Waajiriwa na Wafanya biashara.

Ufugaji wa nyuki kando kando ya Misitu na biashara ya mbao ni miongoni mwa shughuli za kiuchumi zinazokua kwa kasi kwenye Halmashauri ya Wilaya Missenyi

Aidha, kilimo cha umwagiliaji, kilimo cha miwa na alizeti ni miongoni mwa shughuli za kiuchumi ziazoendelea kuhimizwa na kupata mwitikio chanya.

Wakazi wengi walioajiriwa wanafanyakazi kwenye kiwanda cha sukari (Kagera Sugar Co.),Taasisi za Serikali na Watu binafsi zilizomo kwenye Halmashauri.

Wafanya biashara wengi wako kwenye Miji ya Bunazi, Kyaka na Mutukula ambayo inakuwa kwa kasi kubwa.

Pamoja na shughuli zinazoendelea, kuna fursa nyingi za Uwekezaji, hasa kwenye nyanja za Viwanda, Kilimo, Ufugaji, Biashara mipakani na Utalii.

1.3.7.1 Fursa za uwekezaji

Wilaya ya Missenyi imebahatika kuwa na Rasilimali nyingi ambazo zikitumika vizuri zitawaletea Wananchi maendeleo ya haraka na hatimaye maisha bora kwa kila Mwananchi.

Kwa kuwa Rasilimali nyingi hazijaendelezwa vya kutosha, Wilaya inawakaribisha Wawekezaji wa ndani na nje kuja kuwekeza kwenye maeneo yafuatayo:

- Kilimo cha Umwagiliaji kwenye mabonde ya mito ya Kagera na Ngono na mabonde ya Byeju
- Viwanda vya kuchakata maziwa, nyama, ngozi na mazao ya kilimo na uvuvi
- Ujenzi wa Soko la mpakani Mutukula na Majengo mengine ya biashara ndani ya Wilaya.

- Viwanda vya kuchakata mazao ya kilimo (alizeti, mpunga na mahindi)

Uwekezaji huu utawawezesha Wananchi wengi wa Missenyi kujiajiri na Halmashauri pamoja na Serikali kuu zitaongeza mapato yatokanayo na shughuli hizo

1.3.7.1 Kuongeza kipato kwenye kaya maskini

Wilaya ya Missenyi ni miongoni mwa Wilaya zilizopata Mradi wa TASAF III ambapo Kaya maskini 6,298 kati ya Kaya 6,398 zilizolengwa zimetambuliwa. Hatua inayofuata ni kupitia Kaya zote na kuthibitisha utambuzi huo kabla ya kupewa fedha za kuongeza kipato na hatimaye kushiriki kwenye shughuli za maendeleo na ujenzi wa Taifa kwa ujumla.

SURA YA II

UCHAMBUZI KISEKTA

2.0 Utangulizi

Sura hii inatoa uchambuzi wa kina wa nyakati zilizopita na wakati uliopo kwenye Halmashauri ya Wilaya Missenyi. Inachambua pia fursa, changamoto, madhaifu na nguvu zilizopo kwenye Halmashauri.

Hatimaye, Halmashauri itabuni mikakati mbali mbali inayoweza kuondoa madhaifu na changamoto zilizopo pamoja na mbinu zinazoweza kutumia fursa zilizopo kuendeleza Halmashauri

2.1.0 Mapitio ya huduma za Kiuchumi na Kijamii

Kama Halmashauri zingine Tanzania, Halmashauri ya Wilaya Missenyi inakabiliwa na changamoto nyingi za kiuchumi na kijamii kutokana na sababu nyingi, miongoni mwao ni: Kutokuwa na Technolojia ya kisasa, Ukosefu wa rasilimali fedha na mitaji, Kukosekana kwa miundo mbinu ya kiuchumi, Kasi ya ongezeko la watu, Mfumo hafifu wa masoko na Vijana kukimbilia mijini

2.1.1.0 Huduma za Kijamii

Halmashauri ya Wilaya Missenyi inatoa huduma mbali mbali kwa Wadau wake wakiwemo: Jamii, Wafanya biashara, Taasisi za Serikali na za kifedha, Taasisi za kidini, Asasi zisizo za Kiserikali, Makundi mbali mbali ya kijamii, Wakulima, Vikundi vya Ushirika na Watoa huduma wengine.

Mapitio ya sasa ya utoaji wa huduma hizi kwa kila Sekta/Idara na Kitengo ni kama ifuatavyo:

2.1.1.1 Elimu

Huduma za elimu zinazotolewa kwenye Halmashauri ni za aina mbili: Elimu ya Msingi na Sekondari. Hali halisi kwa kila aina ya elimu ni kama ifuatavyo:

Elimu ya Msingi

Wilaya ya Missenyi ina jumla ya Shule 103 za Msingi, zenye jumla ya Wanafunzi 32,609 (wavulana 16,189 na wasichana 16,420). Shule 8 zinazomilikiwa na watu binafsi zina Wanafunzi 1,042 (wavulana 535 na wasichana 507) na za Serikali 95 zina Wanafunzi 31,567 (wavulana 15,654 na wasichana15,913). Asilimia 75 ya darasa la VII waliotahiniwa 2014 walipata nafasi ya kuendelea na masomo ya kidato cha I, 2015

Kuna jumla ya madarasa 621 kati ya 981yanayohitajika, ambayo ni sawa na uwiano wa 1:57 badala ya 1:40. Kuna madawati 12,860 kati ya 19,107 yanayohitajika, ambayo ni sawa na uwiano wa 1:3 badala ya 1:2.

Matundu ya vyoo ni 1,024 kati ya 2,017 yanayohitajika ambayo ni sawa na 1:34 Kwenye shule za msingi kuna jumla ya vitabu 119,499 ambayo ni sawa na uwiano wa 1:4 ikilinganishwa na 1:2

Kwa mwaka 2013, hakuna wanafunzi walioacha masomo

Kuna watu wazima 33,641 (me 11,326 na ke 22,315) wasiojua kuandika, kusoma na kuhesabu (KKK).

Wanafunzi waliosajiliwa kuanza darasa la I, 2013 walikuwa 6,166 (wav. 3,135 na was. 3,031, sawa na asilimia 100 ya watoto waliotarajiwa

Halmashauri ya Wilaya Missenyi ina jumla ya walimu 830 (wanaume 483 na wanawake 347), kati yao kuna wenye cheti, 804 (wanaume 462 na wanawake ni 342) wenye Diploma 18 (wanaume 14 na wanawake 4) na 8 wana digrii (wanaume 7 na wanawake 1). Hii ni sawa na 1:42 ikilinganishwa na ya serikali ambayo ni 1:40.

Kuna nyumba 230 za walimu kati ya nyumba 781 zinazohitajika, ambayo ni sawa na uwiano wa 1:4 badala ya 1:1

Elimu ya Sekondari
Shule za Sekondari ziko 27 (5 za watu binafsi na 22 ni za Serikali) zenye jumla ya wanafunzi 8,686. Kati ya hao; Wanafunzi 6,712 (wavulana 3,262 na wasichana 3,450) ni wa shule za Serikali na Wanafunzi 1,974 (wavulana 1,016 na wasichana 958) ni shule za watu binafsi. Kiwango cha ufaulu mwaka 2014 kimefikia asilimia 37.3 ambapo kati ya watahiniwa 983, watahiniwa 367 wamefaulu kuendelea na kidato cha 5. Kwa kushirikiana na Wananchi, Wilaya ina mpango wa kuanzisha miundo mbinu ya kidato cha V na VI Tarafa ya Kiziba mwaka 2016
Kuna madarasa 220, viti 8,405 na meza 8,393. Kwa sasa hakuna upungufu wa viti wala meza
Kwenye shule za sekondari kuna matundu ya vyoo 311 kati ya 545 yanayohitajika.
Walimu ni 333 (wanaume ni 244 na wanawake 89) kati ya 471 wanaohitajika, wenye diploma ni 180 (wanawake ni 40 na wanaume ni 140) wenye digrii ni 143 (wanaume 97 na wanawake 46) na wenye digrii ya uzamili ni mwanamume 1
Wanafunzi walioacha masomo mwaka 2013 walikuwa 14 (wasichana 8 na wanaume 6) na sababu kuu zilikuwa ni: Utoro wa muda mrefu na shughuli za kujikimu.
Katika kutekeleza Agizo la Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dakt. Mrisho Jakaya Kikwete la kujenga maabara 3 kwenye kila shule; Wilaya ya Missenyi imekamilisha vyumba 3, Vyumba 45 viko hatua ya ukamilishaji, Vyumba 9 viko hatua ya kuezeka na Vyumba 9 viko hatua ya Linta
Wilaya mwaka 2015 inategemea kufungua kidato cha V kwenye shule ya Sekondari Bunazi kwa kusajili Mikondo 2 ya tahasusi za: HKL na KLF yenye jumla ya wanafunzi 70

2.1.1.2 Huduma za Afya
Wananchi wa Wilaya ya Missenyi wanapata huduma ya afya toka kwenye Hospitali mbili: Mgana District Disignated Hospital – Tarafa ya Kiziba na Hospitali ya Kiwanda cha Miwa Kagera – Tarafa ya Missenyi, Kituo cha afya 1 na Zahanati 31 (kati ya hizo, zahanati 3 zinamilikiwa na watu binafsi na Serikali inamilki 28). Zahanati za Ngando (Nsunga) na Kabyaile (Ishozi) ziko hatua ya ukamilishaji
Jumla ya Watumishi wa Afya waliopo ni 318 (Madaktari 16, Wauguzi 182, Wataalamu wa maabara 7, Wafamasia 4, Maafisa Afya 17, Matabibu 25 na Wataalam mtambuka 67) kati ya 665 wanaohitajika
Kada zenye upungufu mkubwa ni pamoja na: Matabibu (25), Maafisa Afya (40), Wauguzi (111 na Wafamasia (28)

Magonjwa 10 yanayosumbua Wilayani Missenyi ni: Malaria, Magonjwa ya njia ya hewa (ARI), Minyoo, Kuhara, Macho, Ngozi, Kichomi (Pneumonia), Ukosefu wa damu (Anaemia), Upasuaji mdogo (Minor Surgical Condition) na Magonjwa ya Zinaa (STDs).

Uboreshaji wa huduma za afya umepewa nafasi kubwa kwenye Mpango Mkakati huu, hasa; Kuongeza idadi ya watumishi, upatikanaji wa Vifaa Tiba na dawa kwenye vituo vyote vya kutolea huduma za afya Wilayani Missenyi

2.1.1.3 Huduma za maji
Wilaya ya Missenyi ina jumla ya miundombinu ya maji 437 inayotoa maji safi kwa wananchi wa Mijini na Vijijini; Visima virefu 65, Visima vifupi 138, Malambo 4, Vyanzo vya maji vya asili 186, Matenki 41 ya kuvuna maji ya mvua na Mito ya

Kagera, Nkenge na Ngono. Kwa sasa, asilimia ya Wananchi wanaopata maji safi ni 53

2.1.2.0 Huduma za Uchumi

Asilimia 85 ya Wakazi wa Wilaya ya Missenyi wanajishughulisha na Kilimo na Ufugaji.

Wilaya ya Missenyi imebahatika kuwa na sehemu kubwa ya ardhí yenye rutuba ya asili, mabonde yenye maji yanayotiririka mwaka mzima pamoja na maeneo yanayofaa kwa ufugaji wa ng'ombe, kuku, kondoo na mbuzi.

2.1.2.1 Kilimo na Ushirika

Kati ya hekta 99,726 zinazofaa kwa kilimo Wilayani Missenyi ni hekta 59,840 sawa na asilimia 60 ndiyo inatumika kwa kilimo cha: Migomba, Mibuni, Maharage, Mahindi, Mpunga, Mihogo, Viazi vitamu, Alizeti, Miwa, Jamii ya kunde na Mboga mboga. Watumishi wa Ugani wako kwenye Kata zote 20 na Vijiji 10 wakitoa elimu ya Kilimo bora na huduma zingine za ugani kwa Wakulima. Kwa sasa kuna upungufu wa Watumishi wa Ugani kwenye Vijiji 67

Maghala ya kuhifadhi mazao yako 29 na masoko ni 8. Juhudi za kuwatafuta Wabia watakaoshirikiana na Halmashauri kujenga Soko la Kimkakati Mpakani (Mutukula) zinaendelea. Hii ni pamoja na kuendeleza Masoko ya Bunazi na Mutukula.

Mabonde na mito inayotiririka mwaka mzima hutoa fursa ya kipekee kwa kilimo cha umwagiliaji, hivyo Wilaya kutokuwa na upungufu wa chakula, huku Wananchi wakijiongezea kipato na ajira ya kudumu.

Wilaya ya Missenyi ina jumla ya SACCOS 36 zenye Wananchama 5,977 na vyama vya Ushirika 34 (Kilimo 30, Mifugo 4)

Kitengo kina jumla ya Watumishi 2 kati ya 10 wanaotakiwa. Upungufu huu husababisha Vyama vya Ushirika na SACCOS kukosa ufuatiliaji wa karibu, hasa katika kukagua mahesabu na kutoa elimu ya usimamizi wa fedha na biashara

2.1.2.2 Mifugo na Uvuvi

Wilaya ina aina nyingi ya mifugo, hasa; Ng'ombe, Mbuzi, Kondoo, Kuku na Nguruwe. Kutokana na Sensa ya Mifugo ya mwaka 2014, kuna Ngombe 68,736, Mbuzi 34,800 Kondoo 546, Kuku 32,501 na Nguruwe 2,932

Kuna Majosho 19, Minada 4, Machinjio 1 na Watumishi wa Ugani 28

Pamoja na idadi hiyo ya mifugo na miundo mbinu yake, bado mahitaji ya nyama na maziwa ni makubwa, hivyo, uwekezaji kwenye ufugaji na viwanda vya kuchakata nyama na maziwa unahitajika zaidi Wilayani Missenyi

Wilaya imepakana na Ziwa Victoria na ni fursa kubwa kwa biashara na uvuvi wa samaki. Kuna jumla ya Wavuvi 58, Mitumbwi 50, Nyavu 1,560 na jumla ya tani 22 huvuliwa kwa mwaka, kati ya tani 25 inayokisiwa kuvuliwa kila mwaka. Watumishi wa Ugani ni 3 kati ya 4 wanaohitajika

2.1.2.3 Miundo mbinu ya Mawasiliano na Nishati

Katika kuwawezesha Wananchi kiuchumi na kijamii, Mawasiliano yanayofanywa kwa njia za: Simu, Barabara, Anga na Maji ni muhimu sana.

Mtandao wa barabara kwenye Wilaya ni km 565.5 (km 193.6 ni za Vijiji na km 371.9 ni za Lami)

Wilaya imetoa eneo sehemu ya Omukajunguti – Kata ya Mushasha (kando kando ya barabara ya lami itokayo Bukoba kuelekea Mutukula kwa Wizara ya Uchukuzi ili ijenge Uwanja wa ndege wa Kimataifa.

Aidha, Halmashauri kupitia Mfuko wa Barabara inaendelea kutenga fedha kila mwaka kwa ajili ya kukarabati barabara zinazounganisha Vijii, Kata, Tarafa na

Wilaya kwa nia ya kurahisisha usafiri na usafirishaji wa mazao ya Wananchi muda wote kwenda kwenye masoko ya ndani na nje ya Nchi.
Wilaya ya Missenyi inaweza kuwasiliana na maeneo mengine kwa urahisi kupitia mitandao ya simu za: TTCL, Voda Com, Airtel, Tigo, Zantel na hata 'Radio calls'.
Wananchi waishio kando kando ya Ziwa Victoria wanatumia usafiri wa kwenye maji kwenda na kusafirisha biashara kwenda: Bukoba, Mwanza au Nchi jirani ya Uganda
Nishati ya umeme kwa sasa inawaka kwenye Wilaya kwa asilimia 60 na jitihada zinaendelea kupitia Mradi wa Umeme Vijijini na ifikapo mwaka 2016 umeme utakuwa unawaka kwenye Kata zote 20
Idara ina jumla ya Watumishi 5 kati ya 8 wanaohitajika kusimamia ukarabati wa barabara, ujenzi wa madaraja na majengo ya Serikali.

2.1.2.4 Maendeleo ya Jamii
Jumla ya Vikundi 240 (Wanawake vikundi 115 na Vijana vikundi 125) vyenye Wananchama 2,400 vimeundwa na kati yao Vikundi 67 (Wanawake vikundi 29 na Vijana vikundi 38) vyenye Wanachama 670 wamepewa mikopo ya Tshs 52,450,000/=. Wilaya ya Missenyi Idara kwa kushirikiana na Kitengo cha Ushirika inatoa elimu ya ushirika na usimamizi wa biashara huku ikiendelea kuwatambua Vijana na Wanawake na kuwapa elimu ya kujiunga kwenye vikundi na kujiongezea kipato
Idara ina jumla ya Watumishi 14 kati ya 25 wanaohitajika na ni Kata 9 pekee ndiyo ina Watumishi wa Maendeleo ya Jamii

2.1.2.5 Misitu, Nyuki na Utalii
Wilaya ina hekta 31,547 za hifadhi ya misitu, sehemu kubwa ikiwa ni Hifadhi ya Misitu ya: Minziro, Mnene, Kikuru, Lwasina, Kantare, Kikongoro, Ruchwezi na Bushenya.
Wananchi anaozunguka misitu hii wanashirikishwa kuhifadhi na kutumia misitu hii kwa kujikwamua kiuchumi, kama vile; Kukata mbao na miti kwa ajili ya kujengea na nishati
Wananchi wanaoishi kando kando ya misitu wamehamasishwa na kuanzisha Vikundi 67 vya ufugaji nyuki na tani 3.2 za asali na tani 1 ya anta huzalishwa kwa mwaka
Kwenye misitu hii kuna wanyama na wadudu wa aina mbali mbali wanaovutia Watalii wa ndani na nje. Msitu wa Minziro unasifika kuwa na wadudu wasiopatikana po pote Tanzania pamoja na nyoka wakubwa sana. Wanyama na Wadudu hawa wakihifadhiwa vizuri wanaweza wakavutia zaidi Watalii na Serikali ikapata mapato ya kutosha
Watumishi wa fani ya ufugaji nyuki hawatoshi kwani yupo mmoja tu ambaye ni Mkuu wa Kitengo badala 2, Watumishi wa Kitengo cha Misitu ni 2 kati ya 6 wanaohitajika.
Kwa sasa hakuna Afisa Utalii japo wanahitajika 2 na kuna fursa nyingi za Utalii kwenye Nyanja za: Misitu, Wanyama na Mambo ya kale

2.1.2.6 Ardhi
Wilaya ina mikakati madhubuti ya kuwawezesha wananchi kurasimisha ardhi yao ili waweze kuitumia kwa ajili ya kukopa au kuweka dhamana kwenye Taasisi za Fedha kwa maendeleo yao.
Kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais (MKURABITA), Wilaya imeweza kupima mashamba 584 kwenye Vijiji 11 (Kata ya Mabale 1, Kassambya 4 Kakunyu 1, Mutukula 2 na Nsunga 3) na Wamiliki wa mashamba hayo wamepewa Hati miliki ya Kimila.

Ili kuondoa migogoro baina ya Wafugaji na Wakulima pamoja na migogoro ya mipaka, Wilaya imepima mipaka ya Vijiji 72 kati ya 77 na inaendelea kuviwezesha Vijiji vingine kuandaa mipango ya matumizi bora ya ardhí kila mwaka.
Halmashauri kupitia Wadau mbali mbali, ina mpango wa kupima na kuendeleza viwanja 1,100 kwenye Miji ya Kyaka - Bunazi – Mutukula pamoja na Miji mingine midogo
Kwa sasa Idara ina jumla ya Watumishi 8 kati ya 14 wanaohitajika

2.1.2.7 Utawala na Utumishi
Idara ina jukumu la kuhakikisha kuwa Watumishi wa kila Kada wanapatikana na kutoa huduma bora na kwa wakati. Hii ni pamoja na Ikama za Idara zote na Vitengo kukamilika. Idara pia huhakikisha kuwa Watumishi wanapata masilahi yao kwa mujibu wa Sheria na Kanuni za kazi
Idara ambazo zina uhaba mkubwa wa Watumishi ni; Afya, Elimu, Uvuvi/Mifugo, Usafi na Mazingira na Utawala.
Halmashauri kwa sasa ina idadi ya Watumishi 5 kati ya 21 wanaotakiwa

2.1.2.8 Mipango
Jukumu kubwa la Idara ya Mipango ni kuratibu shughuli za utekelezaji wa kazi za Halmashauri pamoja na kutoa taarifa mbali mbali ndani na nje ya Wilaya.
Idara pia huunganisha nguvu za Wadau mbali mbali kwa kuwakutanisha na kujadili mikakati ya utekelezaji wa pamoja.ya shughuli za Hamashauri
Idara kwa kushirikiana na Idara na Vitengo vya Halmashauri na Wadau wa maendeleo hufuatilia na kutathmini shughuli za Halmashauri kila baada ya Robo mwaka na baada ya mwaka wa utekelezaji
Idara ina jumla ya Watumishi 3 kwa mujibu wa Ikama.

2.1.2.9 Fedha na Biashara
Kwa mujibu wa Waraka wa Fedha za Serikali za Mitaa (LGA Financial Memorandum) wa mwaka 1997, Idara ya Fedha na Biashara inatekeleza majukumu yafuatayo:

- Kutoa ushauri wa masuala yote ya fedha
- Kubuni vyanzo vya mapato
- Kukusanya na kutunza fedha za Halmashauri
- Kusimamia matumizi ya fedha
- Kuandaa na kuwasilisha taarifa za fedha za kila mwezi/robo mwaka na mwaka
- Kutunza kumbumbuku za fedha na mali zote za Halmashauri

Idara ina jumla ya Watumishi 14 kati ya 20 wanaotakiwa

2.1.2.10 Ukaguzi wa ndani
Kama ilivyo Idara ya Fedha na Biashara, Kitengo cha Ukaguzi wa ndani pia hutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Waraka wa Fedha za Serikali za Mitaa wa mwaka 1997. Miongoni mwa majukumu yake ni pamoja na;

- Kuishauri Halmashauri njia bora za makusanyo na matumizi ya fedha
- Kufanya ukaguzi wa matumizi ya fedha.

Kitengo kina Watumishi 2 kwa mujibu wa ikama

2.1.2.11 Sheria
Halmashauri kupitia Kitengo hiki inahakikisha kuwa shughuli zote zinatekelezwa kwa kufuata Sheria, Kanuni na Utawala Bora.

Aidha, Kitengo cha Sheria kinaondoa malalamiko ya kisheria na kuhamasisha Utawala bora miongoni mwa Jamii ya Missenyi, hatimaye kuwa na ulinzi shirikishi wa kudumu wa Raia na mali zao.
Kitengo kina Mtumishi mmoja badala ya 2 wanaotakiwa

2.1.2.12 Manunuzi (PMU)
Kitengo kinatekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Sheria ya Manunuzi ya 2004 na Kanuni ya 2005.
Miongoni mwa mujukumu hayo ni pamoja na:

- Kuhakikisha Halmashauri inafuata na kutekeleza kwa vitendo Sheria na Kanuni za manunuzi
- Kutunza kumbu kumbu na orodha ya Wazabuni na Wakandarasi wanaofanya kazi kwenye Halmashauri
- Kuitaarifu Halmashauri mienendo ya Wakandarasi na Wazabuni kwa nia ya kuchukua hatua dhidi ya wanaokiuka Mikataba ya kazi zao

Kitengo kina Watumishi 4 kati ya 6 wanaohitajika

2.1.2.13 Teknolojia, Habari na Mawasiliano (TEHAMA)
Kuazishwa kwa mifumo ya kiteknolojia ya mawasiliano kwenye Halmashauri kumepelekea kuwa na Wataalamu wanaowezesha mifumo hii kurahihisha mawasiliano na sehemu zingine za Nchi.
Halmashauri imeanzisha Tovuti na ina barua pepe kwa ajili ya mawasiliano. Pia Ofisi za Mkurugenzi Mtendaji zimewekewa mtandao wa intaneti, ‘Lawson’ kwa ajili ya kurekebisha mishahara na ‘Epicor’ kwa ajili ya kufanya malipo.
Pamoja na mitandao hii kuwepo kwenye Halmashauri, Kitengo kinakosa Mtaalamu wa fani ya IT na sasa kuna Mtumishi mmoja wa fani ya Habari

2.1.2.14 Uchaguzi
Halmashauri kama chombo cha Wananchi, husimamia chaguzi zote za Serikali za Mitaa na kushirikiana na Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) kuendesha Uchaguzi Mkuu wa Rais, Wabunge na Madiwani
Kitengo hiki kinaratibu shughuli zote na michakato ya uchaguzi kama inavyoelekezwa na TAMISEMI (kwa chaguzi za Serikali za Mitaa) na NEC (kwa chaguzi za Rais, Wabunge na Madiwani).
Jukumu kubwa ni kuhakikisha kuwa Wananchi wote wenye uwezo wa kupiga kura wanashiriki kikamilifu kuwachagua Viongozi wao kwa Demokrasia na Uhuru zaidi
Kuna Mtumishi mmoja kwenye Idara yac Utawala anayeratibu shughuli hizi

2.2.0 Masuala mtambuka
Pamoja na huduma za kijamii, kiuchumi, kitamaduni na kisiasa bado Halmashauri inapaswa kuweka msisitizo na kuweka kwenye mipango yake masuala mtambuka, ambayo yanaathiri kwa kiasi kikubwa maendeleo ya Wananchi. Masuala haya ni: VVU/UKIMWI, Jinsia na Makundi maalum, Usafi na Uhifadhi wa Mazingira na Kuwawezesha Wananchi kiuchumi

2.2.1 VVU/UKIMWI
Kiwango cha maambukizi ya VVU/UKIMWI kwenye Halmashauri ya Wilaya Missenyi ni asilimia 3.4 na wanaopata huduma ya dawa za kufubaza madhara ya VVU/UKIMWI (ARVs) ni 3,253 mwaka 2014.
Juhudi za makusudi zinapaswa kuchukuliwa ili kudhibiti na lupunguza kiwango hiki, kwani madhara ya VVU/UKIMWI, yakiwemo vifo, maradhi ya muda mrefu na mahitaji makubwa ya madawa yanaweza kuathiri uchumi wa Wilaya.

2.2.1 Jinsia na Makundi maalum

Maendeleo ya kweli yanaletwa kwa kuwashirikisha makundi yote kwa usawa, hasa; Makundi maalum kama vile Walemavu, Wavulana na Wasichana na Wanaume na Wanawake.

Kupitia Mpango Mkakati, Halmashauri itaweza kutengeneza fursa na kutenga rasilimali kwa ajili ya kuwawezesha makundi haya kushiriki kikamilifu katika maendeleo yao na ujenzi wa taifa kwa ujumla. Utoaji wa mikopo nafuu ni miongoni mwa juhudi za Halmashauri kuwawezesha Makundi haya.

2.2.2 Usafi na Uhifadhi wa Mazingira

Usafi wa Mazingira na Mabadiliko ya Tabia nchi ni mambo muhimu yanayopaswa kuzingatiwa kwa makini katika kuleta maendeleo endelevu kwenye Halmashauri ya Wilaya Missenyi.

Upandaji wa miti, Uhifadhi wa mazingira na Usafi wa mazingira tunayoishi ni nguzo ya kuwezesha mvua kupatikana kwa uwingi na kupunguza hewa ukaa unaoweza kusababisha ukame na ukosefu wa mvua kwa muda mrefu.

Halmashauri kwa kupitia Idara ya Usafi na Mazingira inahamasisha upandaji miti, kuhifadhi maji ya mito na ya Ziwa Victoria, na kila Kaya kutunza usafi wa mazingira yao. Uchafu utokanao na taka ngumu unaendelea kuwekwa kwenye mashimo na madampo kwa ajili ya kuchomwa na ule wa maji taka kupelekwa mbali na maeneo ya makazi

2.2.3 Kuwawezesha Wananchi kiuchumi

Uchumi wa Wananchi wa Missenyi haujaimarika sana kiasi cha kuwawezesha Jamii kupiga hatua ya Maendeleo na kuboresha maisha yao.

Juhudi za makusudi zinachukuliwa na Halmashauri kuhakikisha kuwa umasikini miongoni mwa Wannchi unapungua kama si kwisha kabisa. Juhudi hizi ni pamoja na:

- Kutengeneza fursa za ajira binafsi
- Kuwakopesha Wanawake na Vijana Mikopo yenye riba nafuu
- Kuwakaribisha Wawekezaji watakaowekeza kwenye kuchakata mazao ya Wakulima kwa nia ya kuongeza thamani ya mazao (Value added)
- Kuboresha kilimo na kuwa kilimo cha biashara
- Kuanzisha na kuendeleza kilimo cha umwagiliaji

Hata hivyo, kuna changamoto ya upatikanaji wa fedha za mikopo na urejeshaji wa mikopo inayotolewa kwa Wanawake na Vijana

2.3 Rasilimali muhimu zilizopo Missenyi

Halmashauri ya Wilaya Missenyi imebahatika kuwa na Rasilimali nyingi ambazo zikitumika vizuri zinaweza kuwakwamua Wananchi kiuchumi na hatimaye kuboresha maisha ya kila Mkazi. Rasilimali hizi ni pamoja na: Watu wenye uwezo wa kufanya kazi, Ardhi yenye rutuba, Misitu, Wanyama, Mito Ngono, Kagera na Nkenge pamoja na Ziwa Victoria.

Kwa sasa rasilimali hizi ama hazijatumika au hazitumiwa ipasavyo kuendeleza na kumwondolea umasikini Mwananchi wa Missenyi.

Ushiriki wa Wananchi kwenye shughuli za uchumi haujawa na mwelekeo wa kuwaondoa kwenye umasikini kwani bado wanatumia rasilimali hizi kwa kujikimu tu na wala si kwa ajili ya kibiashara.

Ukosefu wa mitaji na utaalamu ni kikwazo kikubwa katika kutumia rasilimali zilizopo kuwaondolea umasikini Mwananchi. Zana za uvuvi zilizopo ni duni na Wananchi wengi hawajatambua kuwa ufugaji wa nyuki ni biashara inayolipa na inaweza kuwakwamua Wananchi kwenye umasikini

Mpango Mkakati wa miaka mitano (2014 – 2018) umeweka msisitizo wa matumizi bora ya Rasilimali zilizopo Wilayani kwa ajili ya kuwakwamua Wananchi kiuchumi. Hii ni pamoja na; Kupanua kilimo kwa kubadilisha kilimo cha kujikimu na kuwa kilimo cha biashara (hasa cha kutumia trekta na cha umwagiliaji), Ufugaji wa nyuki, Uhifadhi wa misitu kwa kutokata na kuchoma moto misitu ovyo, Uvuvi wenye tija na rafiki kwa mazingara, Kuhifadhi Wanyama na Wadudu kwa ajili ya kukuza Utalii na kuhakikisha kila Mwananchi anashiriki kikamilifu katika shughuli za maendeleo kwa kuwashirikisha Jinsia na Makundi Maalum

2.4 Uchambuzi wa Wadau

Matarajio ya Wadau na yanayotarajiwa kutokea iwapo matarajio yao hayatafikiwa ni kama ifuatavyo

Jedwali I: Uchambuzi wa Wadau ***(Tanbihi: Mpangilio kwa umuhimu – J = Ya juu, K = Ya kati na C = Ya chini)***

Jina la Mdau	Matarajio	Yatakayotokea iwapo matarajio hayatafikiwa	Mpangilio kwa umuhimu (J, K & C)
JAMII	• Maisha ya jamii kuboreshwa na huduma za kijamii na kiuchumi kupatikana kwa wakati	- Umasikini kuendelea - Huduma za kiuchumi na kijamii zisizotosheleza	J
WAKULIMA NA WAFANYA BIASHARA	• Mazao ya kilimo kupatikana kwa uwingi na biashara kuwa ya faida • Mtandao wa usafirishaji na mawasiliano kuboreshwa	- Uzalishaji mdogo wa mazao ya kilimo - Uchumi kupungua kutokana na ukosefu wa masoko	J
SERIKALI KUU (WIZARA YA FEDHA, TAMISEMI, IDARA ZINAZOJITEGEMEA, RAS)	• Kutekeleza MKUKUTA III, TASAF III, Mikakati, Sera na Programu zingine za kitaifa • Matumizi mazuri ya Soko la Afrika Mashariki na kuwa na uhakika wa chakula • Utekelezaji wa Ilani ya Chama Cha Mapinduzi, 2015 - 2020 • Uchumi kukua	- Ongezeko la bei ya bidhaa - Mtazamo hasi wa Serikali kwa wananchi	C J
WATUMISHI WA UMMA	• Mazingira bora ya kazi	Utendaji kazi kuzorota na huduma duni kwa	K

Jina la Mdau	Matarajio	Yatakayotokea iwapo matarajio hayatafikiwa	Mpangilio kwa umuhimu (J, K & C)
		wananchi	
NGOs NA WASHIRIKA WA SERIKALI	• Kushirikiana na Halmashauri kutoa huduma bora kwa wananchi	Huduma hafifu kwa wananchi	K
WANASIASA	• Huduma za kiuchumi na kijamii kwa wananchi kuwa bora. • Utekelezaji wa Utawala bora • Utekelezaji Ilani ya CCM 2015 – 2020 kusimamiwa	Wananchi kuwa na Imani na serikali yao	C
VYOMBO VYA HABARI	• Kuwajulisha wananchi mambo mbali mbali ya maendeleo na matukio muhimu	Wananchi kutojua kinachotekelezwa na serikali yao	J
VYUO VYA JUU	• Watumishi wengi kupata nafasi kwenye vyuo vya juu	Kuwa na Watumishi wasio na sifa	J
VYAMA VYA USHIRIKA NA SACCOS	• Kuongezeka kwa masoko na mikopo yenye masharti nafuu	Uchumi wa wananchi kutokua kwa haraka	K
BUNGE LA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA	• Utekelezaji wa utawala bora na utawala wa kisheria	- Kuyumba kwa nchi - Kuongezeka kwa ufisadi	J
KUNDI MAALUM	• Huduma bora kwa Makundi maalum kuboreshwa na kuwa na fursa kwao	Huduma hafifu kwa makundi maalum na kutokuwa na fursa	J
WAFUGAJI	• Uboreshaji wa idadi na ubora wa mifugo na mazao yao	Umasikini kuendelea kuwepo	H
TAASISI ZA KIFEDHA	• Fursa za kukopesha wananchi kuwepo	Umasikini kuendelea kuwepo	C

2.5 UCHAMBUZI WA SAOC (NGUVU, MAENEO YA KUBORESHWA, FURSA NA CHANGAMOTO)

Jedwali II: SAOC

IDARA/ KITENGO	NGUVU	MAENEO YA KUBORESHWA	FURSA	CHANGAMOTO
UTUMISHI NA UTAWALA	• Watumishi wenye sifa na wenye ushirikiano • Uwepo wa sheria ndogo	• Ofisi chache za VEOs & WEOs na vitendea kazi • Uchache wa nyumba za watumishi ngazi zote	• Uwepo wa Ofisi kuu ya halmashauri na Ofisi za kutosha • Uwepo wa sheria Mama • Mfumo wa utawala uliopo hadi Vijijini na Vitongojini • Uwepo wa vyuo vya Kada mbali mbali	• Idadi kikubwa ya wastaafu kulinganish wa na waajiriwa wapya • Uhaba wa vyombo vya usafiri
MIPANGO, UFUATILIAJI NA TAKWIMU	• Mkuu wa Idara ana uzoefu wa kufanya kazi kwenye Halmashauri zaidi ya 20 • Uwezo wa Idara kuratibu uandaaji wa Mpango Mkakati • Uwezo wa Idara kuratibu Idara na Vitengo kwenye Halmashauri	• Uzoefu mdogo wa kuandaa Mpango wa biashara (business plan writing)	• Uwepo wa Tume ya Mipango, Hazina, TAMISEMI, RAS, MKUKUTA III, TASAF III na Sera za Taifa na za Kisekta • Uwepo wa fursa za uwekezaji na Taasisi za kusaidia uwekezaji • Uwepo wa Wadau wa maendelo ndani na nje ya Wilaya	• Halmashauri kuwa na uwezo mdogo wa kuwekeza • Uhaba wa fedha toka Serikali kuu
KILIMO, MASOKO, UMWAGILIAJI NA USHIRIKA	• Idara ina Mkuu wa Idara mwenye uzoefu na watumishi wenye sifa, ushirikiano na mgawanyo	• Kutokuwa na mpango mkakati na ueledi wa kuratibu wadau wa kilimo na ushirika	• Uwepo wa Sera ya Kilimo na Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji na Ushirika, Wadau wa kilimo • Uwepo wa	• Kutokea kwa Majanga na Maafa

IDARA/ KITENGO	NGUVU	MAENEO YA KUBORESHWA	FURSA	CHANGAMOTO
	wa kazi • Malalamiko machache toka kwa Watumishi wa Ugani • Kuna SACCOS, Vyama vya Ushirika na Vikundi vya Wakulima • Kuna Watumishi wa Ugani • Kuna ARCs • Kuna miundo mbinu ya umwagiliaji	• Wakulima wengi wanalima kilimo cha kujikimu na si kibiashara • Kutokuwa na Mfumo thabiti wa Ufuatiliaji na Tathmini kwenye maeneo ya kuboreshwa • Kutokuwa na miundo mbinu ya umwagiliaji,, na viwanda vya kuchakata mazao	viwanda vya zana za kilimo na upatikanaji wa pembejeo • Upatikaji wa mvua za kutosha • Upatikanaji wa ardhi inayolimika	• Uwepo wa masoko ya mazao yasiyo rasmi • Benki ya Ardhi kutojulikana vizuri kwa Halmashari • Uwepo wa magonjwa ya mazao ya kilimo • Ukosefu wa Mitaji kwa wakulima
MIFUGO NA UVUVI	• Idara ina Mkuu wa Idara na watumishi wenye sifa, ushirikiano na mgawanyo wa kazi • Kuna Watumishi wa Ugani na BMUs pamoja na Umoja wa Wafugaji • Uwepo wa maeneo makubwa ya kufugia • Uwepo wa Ziwa Victoria Maoko ya samaki na mazao ya mifugo	• Kutokuwa na mpango mkakati na ueledi wa kuratibu wadau wa uvuvi na mifugo • Uhaba wa viwanda vya kuchakkata mazao ya mifugo Wilayani	• Uwepo wa Nchi za Afrika Mashariki na Nchi za Maziwa MakuuAvailable market in Burundi, Congo and Zambia • Uwepo wa Sera za Uvuvi na Mifugo pamoja na Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi	• Uwepo wa milipuko ya magonjwa ya mifugo • Uwepo wa uvuvi haramu • Uwepo wa migogoro ya Wafugaji na Wakulima • Upotevu wa mavuno ya samaki baada ya kuvunwa • Uhaba wa vitendea kazi

IDARA/ KITENGO	NGUVU	MAENEO YA KUBORESHWA	FURSA	CHANGAMOTO
ARDHI, MALIASILI NA UTALII	• Uwepo wa Mkuu wa Idara mwenye sifa na uzoefu • Uwepo wa Misitu ya asili na ya kupandwa • Uwepo wa Kamati shirikishi jamii za kusimamia Misitu Vijijini	• Kutokuwepo kwa Masjala ya ardhi ya Wilaya • Wilaya kutokuwa na miliki ya ardhi ya kutosha • Wilaya kutofidia viwanja na kupima miji ya Kyaka, Bunazi na Mutukula	• Uwepo wa maeneo makubwa yasiyopimwa • Uwepo wa Sera, Wizara ya Ardhi na Utalii na Vyuo vya Ardhi • Uwepo wa fursa za Uwekezaji	• Majanga n a Maafa ya asili na yaletwayo na binadamu) • Uhaba wa Wataalamu na vitendea kazi • Ukosefu wa Benki ya Ardhi ya Wilaya • Ukosefu
UJENZI	• Uwepo wa Mkuu wa Idara mwenye uzoefu Team has enough working tools • Uwepo wa vitendea kazi na usafiri	• Usimamizi hafifu wa Mikataba ya ujenzi • Ushirikishwaji hafifu wa wananchi kabla na baada ya kutekeleza miradi ya ujenzi	• Uwepo wa Fedha za mfuko wa barabara • Uwepo wa vifaa vya ujenzi • Uwepo wa Wakandarasi • Uwepo wa Wizara ya Ujenzi, TANROAD, TEMESA na Vyuo vya Ufundi	• Uhaba wa Wakanarasi wenye sifa • Uhaba wa watumishi wenye sifa • Majanga na maafa ya asili na yaletwayo na binadamu
MANUNUZI	• Uwepo wa Kaimu Mkuu wa Kitengo na watumishi wa Ugavi wa kutosha	• Muundo wa kazi za Kitengo cha Manunuzi kutofuatwa • Mkuu wa kitengo anakaimu • Mawasiliano hafifu kati ya Kitengo na Idara na Vitengo vingine kwenye Halmashauri	• Uwepo wa sheria na Kanuni za Manunuzi • Uwepo wa PPRA na GPSA • Uwepo wa Wazabuni na watoa huduma mbali mbali	• Halmashauri kutolipa madeni ya Wazabuni kwa wakati • Watoa huduma kutofahamu sheria na kanuni za manunuzi • Uhaba wa vitendea kazi

IDARA/ KITENGO	NGUVU	MAENEO YA KUBORESHWA	FURSA	CHANGAMOTO
FEDHA NA BIASHARA	• Idara ina Mkuu wa Idara na watumishi mwenye sifa na uzoefu • Kuna vyanzo vya mapato vya kutosha • Watumishi wanaofasham u kutumia mfumo wa EPICOR	• Uwepo wa vitendea kazi • Usimamizi hafifu wa makusanyo ya mapato ya ndani • EPICOR kutofanya kazi kwa ufanisi • Idara kutoratibu ipasavyo Idara zinazokusanya mapato ya ndani	• Uwepo wa Mfumo wa malipo (EPICOR), Vyuo vya fedha, Wizara ya Fedha, CAG, NAO, LAAC, Sheria na Kanuni za fedha	• Uhaba wa watumishi wa Kitengo cha Biashara • Walipa ushuru na kodi kutokuwa tayari kulipa na kukosa elimu ya ulipaji kodi na ushuru
MAENDELEO YA JAMII	• Mkuu wa Idara na watumishi mwenye sifa na uzoefu • Idara ina ofisi za kutosha	• Uratibu hafifu wa Wadau wa maendeleo kwenye Wilaya • Kipato kidogo cha wananchi	• Uwepo wa Asasi za kiraia na zisizo za serikali • Uwepo wa Vikundi vya Vijana na Wanawake • Uwepo wa Sera ya Maendeleo ya jamii, Wizara ya Maendeleo ya Jamii, TACAIDS, TASSAF	• Uhaba wa watumishi na vitendea kazi • Ukosefu wa fedha • Marejesho hafifu ya mikopo toka kwenye Vikundi
ELIMU	• Wakuu wa Idara za elimu sekondari na Msingi na watumishi wenye sifa na uzoefu • Mahusiano mazuri kati ya Idara ya elimu msingi na sekondari	• Mazingira yasiyoridhisha ya kazi Vijijini • Uhaba wa vifaa vya kufundishia na kujifunza • Walimu kutopata haki zao za kisheria kwa wakati • Walimu wengi kutojua tofauti	• Uwepo wa fedha za LCDG na Capitation • Uwepo waSera ya Elimu, Wizara ya Elimu na UFUNDI,Vyuo va elimu, TAMISEMI na Vituo vya kujifunzia walimu (TRCs) • Uwepo wa	• Uhaba wa waalimu • Uhaba wa nyumba za walimu • Uhaba wa matundu ya vyoo • Uhaba wa vyumba vya maabara

IDARA/ KITENGO	NGUVU	MAENEO YA KUBORESHWA	FURSA	CHANGAMOTO
	• Idra zina ofisi za kutosha • Kuna shule za msingi kila Kijiji na za sekondari kila Kata • Bodi za shule za sekondari na Kamati za shule za zinazofanya kazi	na uhusiano baina ya Haki na Wajibu kazini	shule za watu binafsi	
USAFI NA MAZINGIRA	• Mkuu wa Idara mwenye sifa na uzoefu • Idara ina ofisi za kutosha	• Kutokuwepo na Muundo wa utumishi kwenye Idara	• Uwepo wa NGOs na Wadau wa Mazingira • Uwepo kwa Sera ya Afya na NEMC	• Uhaba wa vitendea kazi na usafiri wa uhakika • Maafa na majanga • Kutokuwepo kwa viwanda vinavyoweza kuzungusha mabaki ya plastiki • Wananchi kuwa Elimu ndogo juu ya afya na madhara ya uchafu wa mazingira
MAJI	• Mkuu wa Idara mwenye sifa na uzoefu • Idara ina ofisi za kutosha • Idara ina vitendea kazi na usafiri	• Miradi ya maji kutokamlika kwa wakati kutokana na uhaba wa fedha • Miradi ya maji inahitaji mtaji na gharama kubwa ya uendeshaji	• Wizara ya Maji, Sera ya maji na vyanzo vingi vya maji • Uwepo wa vikundi vya watumiaji maji (COWSOs)	• Uhaba wa watumishi • Fedha kutopatikana kwa wakati
AFYA NA USTAWI WA JAMII	• Mkuu wa Idara na watumishi mwenye sifa na uzoefu • Uwepo wa hospitali 2,	• Uhaba wa Zahanati na Vituo vya afya • Ukosefu wa hospitali ya Wilaya	• Uwepo kwa Wizara ya Afya na Ustawi wa jamii, Sera ya afya, TACAIDS, Basket Fund, Wadau wa Afya,	• Milipuko ya magonjwa • Maafa na majanga

IDARA/ KITENGO	NGUVU	MAENEO YA KUBORESHWA	FURSA	CHANGAMOTO
	Kituo cha afya na zahanati 28 • Uwepo wa Timu ya Uongozi wa afya (CHMT) • Uwepo wa vitendea kazi na usafiri	• Uwepo wa watumishi wengi wasio na sifa	NGOs	• Uhaba wa watumishi • Uhaba wa fedha
UKAGUZI WA NDANI	• Mkuu wa Kitengo na watumishi mwenye sifa na uzoefu • Ofisi za kutosha kwa watumishi wote na usafiri • Uwepo wa ratiba ya kuwasilisha taarifa ya ukaguzi kila Robo mwaka	• Uelewa mdogo wa Sheria za fedha miongoni mwa watumishi wa ngazi za Kata na Vijiji • Ugumu wa mawasiliano kati ya Makao makuu na Vijiji na Kata	• Uwepo wa sheria, kanuni na miongozo ya matumizi ya fedha a Serikali za Mitaa • Uwepo wa Idara inayojitegemea ya Ukaguzi, CAG, NAO, TAMISEMI, Wizara ya fedha,Vyuo vya fedha na NBAA	• Uhaba wa fedha na vitendea kazi • Watumishi wa ngazi za Vijiji na Kata kutokuwa na ujuzi wa kufuata taratibu za matumizi ya fedha
SHERIA	• Uwepo wa Kaimu Mkuu wa Kitengo mwenye sifa	• Nafasi ndogo ya kuwaelewesha watumishi na jamii umuhimu wa kufuata sheria (Para Legal)	• Uwepo wa Wizara ya Sheria na Katiba, TAMISEMI, Mahakama, Vyuo vya Sheria, Sheria ndogo za Halmashauri, Polisi, PCCB	• Uhaba wa watumishi na vitendea kazi • Uelewa mdogo wa sheria miongoni mwa Jamii
TEHAMA	• Uwepo wa Kitengo cha TEHAMA • Uwepo wa Kaimu Mkuu wa Kitengo na Msimamizi wa TEHAMA	• Tovuti ya Halmashauri kutoeleweka kwa watumishi na kuchangia kuiboresha kwa matumizi ya watu wengine	• Uwepo mtandao wa Intaneti Bunazi • Uwepo wa Tovuti ya Halmashauri • Uwepo wa TEHAMA Mkoani	• Uhaba wa watumishi na vitendea kazi • Mtandao wa intaneti kutokuwepo kila ofisi

IDARA/ KITENGO	NGUVU	MAENEO YA KUBORESHWA	FURSA	CHANGAMOTO
UCHAGUZI	• Uwepo wa Kitengo kwenye Halmashauri • Uwepo wa Vyama 6 vya Siasa kwenye Wilaya • Uwepo waKaimu Mkuu wa Kitengo	• Baadhi ya Vyama vya Siasa kuendesha shughuli za siasa bila kufuata taratibu • Watumishi kutoelewa sheria za uchaguzi na ushiriki wao kwenye shughuli za siasa	• Uwepo wa Tume ya Uchaguzi, TAMISEMI, Mawasiliano ya simu Wilayani kote	• Vyama vya siasa kutofanya kazi kwa kshirikiana, hasa wakati wa uchaguzi • Ukosefu wa vyombo vya usafiri
NYUKI	• Uwepo wa Kaimu Mkuu wa Kitengo • Uwepo wa misitu ya asili nay a kupanda	• Wananchi wengi hawajaelea umuhimu wa ufugaji wa nyuki kiuchumi	• Uwepo wa Wizara ya Maliasili, Mamlaka ya Kuhifadhi Misitu, Sera na sheria ya kuhifadhi Misitu, Vikundi vya ufugaji nyuki	• Uhaba wa watumishi na vitendea kazi • Uhaba wa fedha

SURA TA III

DIRA, DHIMA, AMALI NA MAENEO YENYE MATOKEO MUHIMU

3.0 Utangulizi

Halmashuri ya Wilaya Missenyi ilipoanzishwa mwaka 2007 iliandaa mwelekeo na Dira yake ambayo itaiongoza kwa muda wote wa kufanya shughuli zake na kuwahudumia Wananchi wake.

Halmashauri ina Dira, Dhima na Amali ambazo kwa pamoja ni mwelekeo mwongozo kamili wa shughuli zake za kila siku.

3.1. Dira

Dira ya Halmashauri ya Wilaya Missenyi inasema: “Kuwa na Wananchi wenye maendeleo endelevu na miundo mbinu na huduma za kiuchumi na kijamii iliyo bora ifikapo 2025”

3.2 Dhima

Dhima ya Halmashauri inasema: “Kuijengea uwezo Jamii na taasisi zake ili kutoa huduma bora za kiuchumi na kijamii kwa kushirikiana na Wadau kwa kuzingatia Utawala Bora”.

3.3 Amali (Core Values)

Ili Halmashauri ya Wilaya Missenyi iweze kurekeleza shughuli zake kwa mafanikio na ufanisi, haina budi kuwa na amali ambazo ni:

- ***Matumizi mazuri ya Rasilimali zilizopo:*** Kuhakikisha rasilimali za Halmashauri zilizopo zinamilikiwa na kutumika kwa kuelekezwa kwenye maeneo muhimu ili kuleta ufanisi na tija ufanisi na tija.
- ***Ushirikishwaji wa Jamii:*** Mafanikio tarajiwa yatapatikana tu pale Jamii watakaposhirikishwa katika ngazi ya maamuzi, utekelezaji na tathmini ya utekelezaji wa miradi yao
- ***Uwajibikaji wa pamoja:*** Watumishi, Viongozi na Jamii wanapaswa kushirikiana na kuwajibika kwa pamoja katika hatua zote ili kuwa nafasi ya kukosoana na kurekebisha makosa kabla ya kupata matunda ya kazi yao
- ***Utawala bora:*** Halmashauri inapaswa kufanya shughuli zake kwa kufuata misingi ya Utawala bora unaozingatia: Uwazi, Ukweli, Demokrasia na Utawala wa kisheria. Hii itawezesha Wananchi na Wadau wengine kuweza kuhoji utendaji wa Halmashauri

3.4 Maeneo yenye matokeo muhimu

Maeneo yenye matokeo muhimu yanayotarajiwa na Halmashauri, Wananchi na Wadau wengine ni pamoja na:

- Kuongezeka kwa mapato ya ndani
- Huduma bora za kiuchumi na za kijamii zinazopatikana kwa wakati
- Ushirikishwaji wa Jamii katika kupanga, kutekeleza, kusimamia na kutathmini utekelezaji
- Matumizi mazuri ya mali za Umma na usimamizi wa rasilimali na maliasili kwa manufaa endelevu ya jamii
- Uwepo wa Utawala bora
- Kutunza amani na usalama wa raia na mali zao

3.4.1 Kuongezeka kwa mapato ya ndani

Halmashauri ya Wilaya Missenyi huendesha sgudhuli zake kwa kutumia fedha zinazotoka Serikali kuu, Wafadhili na Wahisani mbli mbali walioko ndani na nje ya Wilaya pamoja na mapato yake ya ndani, Hata hivyo, juhudi za makusudi huchukuliwa kuongeza mapato ya ndani kwani mapato toka vyanzo vingine hupungua kadri mahitaji yanavyoongezeka.

Kwa msingi huo, Halmashauri inapaswa kuweka mkazo kwenye ukusanyaji wa mapato ya ndani na kubuni vyanzo vingine vipya, Kwa kufanya hivyo, ni wazi kuwa ubora na uwingi wa huduma utadumishwa

3.4.2 Huduma bora za kiuchumi na za kijamii zinazopatikana kwa wakati

Kwa ujumla, huduma za kiuchumi na kijamii kwenye Halmashauri hazijatolewa kwa kiwango bora zaidi, Miundo mbinu za shule, maji, afya na usafi wa mazingira bado haijaboreshwa vya kutosha na uchumi wa Wananchi nao bado uko chini.

3.4.3 Ushirikishwaji wa Jamii

Wananchi wakishirikishwa kikamilifu kwenye hatua ya maamuzi na utekelezaji, ni wazi kuwa miradi yao wataisimamia na kuwanufaisha kwa muda mrefu. Jamii na Viongozi wao wanapaswa kufundishwa na kuhamasishwa ili washiriki kikamilifu kutambua vipaumbele vya mahitaji yao pamoja na kuchangia kwa manufaa yao wenyewe kupitia dhana ya Fursa na Vikwazo katika Maendeleo (O & OD).

3.4.4 Matumizi mazuri ya mali za Umma na usimamizi wa rasilimali na maliasili

Halmashauri ya Wilaya Missenyi imebahatika kuwa na maliasili nyingi kama vile; Misitu, Milima, Mabonde, Ardhi, Wanyama pori, Ziwa Victoria na Mito. Halmashauri inategemea kutumia rasilimali hizi kwa maendeleo ya Wananchi.

3.4.5 Uwepo wa Utawala bora

Halmashuri kwa sasa inatekeleza nguzo ya Utawala bora kwa kuimarisha: Demokrasia, Uwazi na ukweli, Ushirikishwaji wa Jamii na Utawala wa kisheria

3.4.6 Kutunza amani na usalama wa raia na mali zao

Maendeleo ya kweli yatapatikana kwa Wananchi panapokuwa na amani na usalama wao na mali zao. Halmashauri inafanya kila liwezekanalo kusimamia kwa nguvu zote amani ya Wananchi na usalama wao na mali zao ili washiriki kikamilifu katika kujiletea maendeleo yao

3.5 Madhumuni ya Halmashauri

Kwa muda wa utekelezaji wa Mpango Mkakati, Halmashauri itatekeleza madhumuni makuu yafuatayo:

A. Huduma kuboreshwa na kupunguza maambukizi ya VVU/UKIMWI
B. Mikakati ya kupambana na Rushwa kutekelezwa
C. Huduma bora kutolewa kwa usawa
D. Ubora na uwingi wa huduma na miundombinu kuongezwa
E. Utawala bora kufuatwa
F. Ustawi wa Jamii, Jinsia na kuwawezesha Jamii
G. Usimamizi wa dharura na majanga kuboreshwa

SURA YA IV

MALENGO NA UTEKELAZAJI WA MPANGO MKAKATI KWA MIAKA 5

4.0 Utangulizi

Jedwali la III linaonesha uhusiano uliopo kati ya tatizo, dhumuni, lengo na mikakati inayotakiwa kuondoa tatizo miongoni mwa jamii na kuleta maendeleo ya kiuchumi, kijamii, kisiasa na kiutamaduni. Jedwali pia hutoa viashiria na mhusika mkuu katika utekelezaji wa mikakati hiyo.

Kutokana na jedwali hili, Halmashauri itaandaa kazi za kufanya kutokana na mikakati kwa kila Idara na Kitengo, ambapo kazi hizo zitaendana na bajeti itakayohitajika kugharamia utekeleazi wa kazi hizo.

Kazi zikiandaliwa kwa makini na kuelekeza rasilimali kwenye utekelezaji wenye tija, Halmashauri itapiga hatua ya maendeleo na kuondoa kero kwa wananchi ndani ya muda maalum ya utekelezaji wa Mpango Mkakati

Jedwali III: MALENGO NA MIKAKATI YA UTEKELEZAJI WA MPANGO MKAKATI 2014 – 2018

IDARA YA ARDHI NA MALIASILI

Tatizo	Dhumuni	Lengo	Mikakati	Viashiria	Mhusika
Ujenzi holela katika miji ya Kyaka – Bunazi na Mutukula	Kuboresha upatikanaji na utoaji huduma bora za makazi kwa jamii.	Kupima viwanja 1,000 ifikapo mwaka 2018.	1. Kuwa na mpango kamambe (Interim Land Use Plan) wa kuendeleza miji ya Kyaka-Bunazi na Mutukula. 2. Kuimarisha mahusiano na Taasisi za fedha kwa ajili ya kukopa.	Idadi ya nyumba zilizojengwa kwa kufuata mipango miji Idadi ya viwanja vilivyopimwa kwa mwaka. Idadi ya waombaji wa viwanja	Afisa Ardhi na Maliasili Jamii Viongozi ngazi zote
Migogoro ya ardhi ndani ya vijiji		Kuandaa Mpango wa matumizi bora ya ardhi Vijiji vyote 20 ifikapo 2018	1. Kuimarisha utendaji kazi wa mabaraza ya ardhi ya Kata 2. Kuimarisha mahusiano na Taasisi za fedha kwa ajili ya kukopa.	Idadi ndogo ya migogoro ya ardhi Vijijini.	Afisa Ardhi na Maliasili Mabaraza ya Kata na Jamii
Uharibifu wa mazingira na uvunaji haramu wa misitu ya hifadhi pamoja na uchomaji moto ovyo	Misitu ya Serikali na ya asili kulindwa na kuhifadhiwa	1. Kupanda miti 7,500,000 Ifikapo mwaka 2018 2. Kudhibiti uvunaji haramu wa misitu na uchomaji misitu toka asilimia 60 hadi 80 ifikapo Juni, 21018	1. Kuwa na Kamati za mazingira zinazowajibika 2. Kuwa na doria kwenye misitu yote. 3. Dhana ya Usimamizi wa Misitu Shirikishi (PFM) kuenezwa kwenye Vijiji vyote vinavyozunguka misitu 4. Uanzishwaji wa vitalu vya miche ya miti	Idadi ya miti inayopandwa Idadi ya Kamati za Mazingira Idadi ya doria Idadi ya vitalu vya miche	Afisa Ardhi na Maliasili NGO/CSOs Taasisi za Umma na Binafsi Jamii

KITENGO CHA NYUKI

Tatizo	Dhumuni	Lengo	Mikakati	Viashiria	Mhusika
Ufugaji wa nyuki kutopewa umuhimu unaostahili	Ufugaji wa nyuki kuwa shughuli ya kiuchumi	Kuongeza idadi ya Wafugaji nyuki kutoka vikundi 58 hadi 72 ifikapo Juni 2018.	1. Kushirikisha jamii na wadau mbalimbali kwa kutoa elimu ya ufugaji nyuki katika Vijiji vyote 2. Kuimarisha na kuunda vikundi vingine vya ufugaji nyuki (wenye sumu na wasio na sumu).	idadi ya vikundi vilivyoanzishwa Idadi ya Mizinga ya nyuki Tani za Asali na Nta iliyozalishwa	A/Ufugaji nyuki,NGOs, Na CBO na wananchi

IDARA YA KILIMO, UMWAGILIAJI NA USHIRIKA

Tatizo	Dhumuni	Lengo	Mikakati	Viashiria	Mhusika
1. Utoaji wa huduma za ugani zisizoridhisha	Utoaji wa huduma bora za ugani kwa wakulima kwenye Vijiji vyote	Huduma bora za ugani kuboreshwa toka 30% hadi 60% ifikapo Juni 2018.	1. Kuwa na Maafisa Ugani kila Kijiji 2. Maafisa Ugani kuwa na vitendea kazi 3. Vituo vya Wakulima kuboreshwa 4. Wakulima kushindanishwa kupitia maonesho na mashamba darasa	Idadi ya Maafisa Ugani ngazi ya Kijiji/Wilaya Idadi ya Maafisa Ugani wenye vitendea kazi Idadi ya vituo vya Wakulima vilivyoboreshwa Idadi ya Wakulima walioshinda tuzo	Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji na Ushirika Halmashauri
2. Uhaba wa miundo mbinu bora ya masoko na maghala ya mazao ya kilimo.	Kuwa na miundo mbinu bora ya masoko na maghala kila Kata	1. Kuongeza masoko ya mazao ya kilimo toka 7 hadi 10 ifikapo Juni, 2014 2. Kuongeza maghala ya mazao ya kilimo toka 4 hadi 7 ifikapo Juni, 2014	1. Ushirikishwaji wa Wananchi katika kujenga miundo mbinu ya masoko na maghala 2. Kuelimisha zaidi Wananchi dhana ya Mpango wa DADPs 3. Kuwa na mfumo mzuri wa ufuatiliaji ngazi zote	Idadi ya masoko yaliyojengwa/karabatiwa Idadi ya maghala yaliyojengwa/ karabatiwa Idadi ya Vikundi vya Wakulima vilivyofuatiliwa	Wakulima Halmashauri Vikundi vya Wakulima NGOs Wizara ya Kilimo Viongozi ngazi zote
3. Tishio la Usalama na uhakika wa chakula kwenye Kaya	Kuwa na usalama na uhakika wa chakula kwenye Kaya zote Wilayani	Uzalishaji wa mazao ya chakula kuongezeka toka tani 2.5 hadi 3.5 kwa Ha. ifikapo Juni, 2018	1. Kuwa na Wawekezaji kwenye kilimo cha Umwagiliaji 2. Wakulima kupata huduma za ugani toka kwa Wawekezaji 3. Kuanzisha Vikundi vya Wakulima 4. Kutokomeza ugonjwa wa migomba 5. Kuhamasisha kilimo cha mboga mboga	Idadi ya skimu za umwagiliaji Idadi ya Wakulima wanaopata huduma za ugani Idadi ya migomba iling'olewa na mipya iliyopandwa Idadi ya Ha. za mazao ya mboga mboga zilizolimwa	Wawekezaji Vikundi vya Wakulima
4. Wilaya kuendelea kutegemea		Tani 300 ya Mazao ya Alizeti, Ulezi na Shayiri kuzalishwa	1. Kuanzisha mashamba darasa ya mazao mapya 2. Kutoa elimu kwa Wakulima na	Idadi ya Mashamba darasa Idadi ya Wakulima waliopata	Halmashauri Wakulima

mazao ya Mibuni, Miwa na Migomba kama mazao ya Biashara	Wilaya kuwa na mazao zaidi ya Biashara	ifikapo Juni, 2018	Vikundi vya Wakulima kuhusu umuhimu wa mazao ya Shayiri, Ulezi na Alizeti Kuwakaribisha Wawekezaji wa kilimo cha Alizeti, Shayiri na Ulezi	elimu Idadi ya Wawekezaji wanaolima Alizeti, Shairi na Ulezi Idadi ya Ha. zilizolimwa	Halmashauri Global Agency
5. Uzalishaji wa Mazao ya Mibuni na Migomba kupungua	Uzalishaji wa Mazao ya Mibuni na Migomba kuongezeka	1. Uzalishaji wa zao la Mibuni kuongezeka toka Kg 400 hadi Kg 500 kwa Ha. ifikapo Juni, 2018	1. Wakulima kupanda miche mipya 2. Wakulima kupata huduma za ugani na pembejeo kwa wakati	Idadi ya miche mipya iliyopandwa Idadi ya Wakulima waliopata pembejeo	Wizara Wakulima wa mibuni/migomba Halmashauri TACRI
		2. Uzalishaji wa zao la Migomba kuongezeka toka Tani 5 hadi Tani 7.5 kwa Ha. ifikapo Juni, 2018	1. Wakulima kupanda miche mipya 2. Wakulima kupata huduma za ugani na pembejeo kwa wakati		
6. Kilimo cha Miwa kutotoshelez a mahitaji ya Kiwanda cha Sukari Kagera	Wakulima kuzalisha kwa wingi zao la miwa	Uzalishaji wa zao la miwa kuongezeka toka Tani 30 hadi Tani 45 kwa Ha. ifikapo Juni, 2014	Wakulima kupewa huduma za ugani na pembejeo kwa wakati Wakulima kupanda miche bora	Idadi ya Tani zilizozalishwa Idadi ya Miche iliyopandwa Idadi ya Wakulima waliopata huduma za ugani na pembejeo	Wakulima Halmashauri Maafisa Ugani KASGA Kagera Sugar
7. Mazao yanayozalish wa kutokuwa na bei nzuri	Mazao ya Biashara yanayozalishw a Wilayani kuongezewa thamani kabla ya kuuzwa	1. Kujenga viwanda 4 vya kuchakata Alizeti, Mpunga, Mahindi na Shayiri ifikapo Juni, 2014	1. Kuwakaribisha Wawekezaji kujenga Viwanda vya kuchakata Mpunga, Mahindi, Shayiri na Alizeti 2. Kuwa na eneo moja Mutukula kwa ajili ya kuuza mazao ya kilimo	Idadi ya Viwanda vilivyojengwa	Halmashauri Wananchi, Vikundi vya wakulima Wawekezaji

8. Vikundi vya Wakulima vichache na dhaifu	Wilaya kuwa na Vikundi vya Wakulima/ Ushirika vingi, imara na vyenye mitaji	Kuongeza idadi ya Vyama vya Ushirika Wakulima toka 73% hadi 83% na Vyama vya Wakulima toka 40% hadi 50%ifikapo Juni, 2018.	1.Kufikisha elimu ya Ushirika kwenye Kata zote 2. Kuhakikisha Vyama vya Ushirika na vya Wakulima vilivyopo vinaunda SACCOS 3. Kuwezesha Vyama vya Ushirika na vya Wakulima kukopa kwenye Taasisi za fedha	Idadi ya Kata zilizopata elimu ya vyama vya ushirika Idadi ya Vyama vya Ushirika vilivyoanzisha SACCOS Idadi ya Vyama vya Ushirika vilivyokopa kwenye Taasisi za Fedha	Afisa Ushirika Vyama vya Ushirika Taasisi za Fedha

IDARA YA UJENZI

Tatizo	Dhumuni	Lengo	Mikakati	Viashiria	Mhusika
Kutopitika kwa barabara katika kipindi chote cha mwaka	Ubora wa huduma za kiuchumi na miundo mbinu kuongezeka	Matengenezo ya barabara toka Km 250 hadi Km 565 ifikapo Juni 2018	1. Kuimarisha uwezo wa watumishi wanaosimamia kazi za barabara 2. Kujenga mahusiano mazuri na wakandarasi 3. Elimu kwa umma kuhusu utunzaji wa barabara 4. Kupata wakandarasi wazoefu na wenye mitaji 5. Wasimamizi wa miradi ngazi ya Kata na Vijiji kuwezeshwa	Idadi ya km za barabara zitakazojengwa Idadi ya km za lami zitakazojengwa Idadi ya madaraja/kalvat yatakayojengwa	Wananchi wote, Wakandarasi, Watumishi wa Ujenzi WEOs VEOs
		Matengenezo ya Km 6 za lami katika Miji ya Bunazi na Mutukula ifikapo Juni, 2018			
		Matengenezo ya kalvati/madaraja 100 ifikapo Juni 2018			
Viwango hafifu vya majengo yanayojengwa Vijijini		Viwango vya majengokuimarishwa kwenye Vijiji vyote toka 60 hadi 80 ifikapo June 2018			

KITENGO CHA MANUNUZI

Tatizo	Dhumuni	Lengo	Mikakati	Viashiria	Mhusika
Huduma isiyoridhisha kwenye Halmashauri	Watoa huduma kutoa huduma bora kwenye Halmashauri	Huduma za manunuzi kwenye Halmashauri kuboreshwa toka asilimia 50 hadi 70 ifikapo Juni, 2018	1. Watoa huduma kwenye Halmashauri kujua umuhimu wa huduma zao na Wajibu wao 2. Kuwa na mahusiano mazuri kati ya Mtoa huduma na Halmashauri	Idadi ya watoa huduma bora na kwa wakati	Halmashauri Watoa huduma.

IDARA YA MIFUGO NA UVUVI

Tatizo	Dhumuni	Lengo	Mikakati	Viashiria	Wahusika
1. Kuenea kwa magonjwa, uhaba wa vyakula vya mifugo na mazao duni ya mifugo.	1. Kuongeza uzalishaji wa mazao bora ya mifugo yanayokidhi viwango vya soko la ndani na nje	1. Kudhibiti magonjwa ya mifugo toka 55% hadi 85% ifikapo Juni, 2018.	1. Kutoa tiba na kinga kwa chanja mifugo dhidi ya magonjwa. 2. Wafugaji kupewa elimu ya ufugaji bora na wenye tija	I. Magonjwa ya mifugo kupungua. II. Wafugaji waliopewa elimu ya ufugaji wenye tija	Wizara ya Mifugo/Uvuvi, Halmashauri ya Wilaya. Watoa huduma binafsi, Wafugaji, Wafadhili Wananchi Viongozi wa Kata na Vijiji
2. Mazao ya mifugo hafifu	1. Mazao ya mifugo kuboreshwa na thamani kuongezeka.	2. Kuboresha koosafu za mifugo ya asili toka 30% hadi 60% ifikapo Juni, 2018.	1. Uhamilishaji wa mifugo	Tani ya mazao ya mifugo	
		3. Kupatikana kwa malisho na vyakula bora vya ziada toka 55% hadi 80% ifikapo Juni, 2018.	1. Kuwezesha Wananchi kuwa na Mpango wa matumizi bora ya ardhi kutenga ardhi kwa ajili ya malisho ya mifugo. 2. Kuhamasisha uanzishwaji wa viwanda vidogo vya kusindika vyakula vya mifugo	Idadi ya Vijiji vyenye mpango wa matumizi bora ya ardhi	
		4. Kuanzisha viwanda 3 vya kuchakata mazao ya mifugo (ngozi, nyama na maziwa) Wilayani ifikapo Juni, 2014	1. Kuwahamasisha Wawekezaji wa Sekta ya Mifugo	Idadi ya Viwanda vya kuchakata mazao ya mifugo	Wawekezaji Wafugaji Halmashauri
3. Ongezeko la uvuvi haramu	1. Kuthibiti uvuvi haramu na kuhimiza uvuvi wa tija na rafiki wa mazingira	2. Kuongeza elimu ya uvuvi kwa wavuvi na wafugaji samaki toka 45% hadi 80% ifikapo Juni 2018.	1. Kutoa mafunzo ya uvuvi bora na wenye tija kwa Wavuvi. 2. Kuhamasisha ufugaji wa samaki kwa kutoa elimu 3. Kuzishirikisha BMU kusimamia uharibifu wa mazingira	Idadi ya matukio ya uvuvi haramu. Idadi ya Mabwawa	Halmashauri Wavuvi BMU

IDARA YA MAENDELEO YA JAMII

TATIZO	DHUMUNI	LENGO	MIKAKATI	VIASHIRIA	MHUSIKA
1. Kipato kidogo kwa jamii hasa Wanawake na Vijana	Kuongeza kipato kwa Jamii, hasa Wanawake, Vijana na Makundi maalum	1.Kuanzisha miradi ya kiuchumi kwa Wanawake, Vijana na Makundi maalum toka vikundi vya Wanawake 33 hadi 120, Vijana toka 26 hadi 96 na Makundi maalum toka 4 hadi 10 ifikapo Juni, 2018	1. Kuwa na mipango inayoimarisha na kuendeleza miradi ya vikundi vya kiuchumi vya Wanawake, Vijana na Makundi maalum	Idadi ya vikundi vilivyoanzisha miradi	Halmashauri, JAMII, NGOs CBOs CSOs
2. Wanawake kutokuwa na uelewa juu ya sheria za kumiliki ardhi na mirathi	Kuwezesha Wanawake kupata ufahamu wa sheria ya ardhi na mirathi	2. Kuwezesha vikundi vya Wanawake kupata elimu ya umiliki wa ardhi na mirathi kutoka vikundi 80 hadi 160 ifikapo Juni, 2018	1. Kuwa na mipango inayoelimisha na kuimarisha usawa kijinsia katika jamii	idadi ya vikundi vilivyopata elimu	
3. Ukosefu wa mitaji ya kuendesha shughuli za kiuchumi kwa vikundi vya wanawake na vijana	Kuongeza mitaji ya vikundi vya kiuchumi	3. Kutoa mikopo kwa vikundi vya kiuchumi vya Wanawake kutoka 33 hadi 72 na vikundi vya Vijana kutoka vikundi 26 hadi 66 ifikapo Juni, 2018	1.Kuwa na mipango inayoimarisha na kuendeleza miradi ya vikundi vya kiuchumi vya wanawake na vijana	Idadi ya vikundi vilivyopata mikopo	
4. Uelewa mdogo juu ya uendeshaji wa miradi ya kiuchumi na ujasiriamali	Kuongeza uelewa juu ya uendeshaji wa miradi ya kiuchumi kwa vikundi vya wanawake na vijana	4. Kuelimisha vikundi vya Wanawake kutoka 60 hadi 120 na Vijana 60 hadi 120 juu ya elimu ya uendeshaji wa miradi ya kiuchumi na ujasiriamali ifikapo Juni, 2018	Kujenga uwezo kwa Vikundi vya kiuchumi vya wanawake na vijana kujengewa uwezo juu ya ujasiriamali na uendeshaji wa miradi ya kiuchumi	Idadi ya vikundi vilivyopata elimu ya ujasiriamali	
5. Watoto wanaoishi kwenye Mazingira magumu kutopata huduma	Watoto wanaoishi kwenye mazingira magumu kupata huduma za Jamii	Watoto wanaoishi kwenye mazingira magumu wanaopata huduma za jamii kuongezeka toka 30 hadi 100 ifikapo Juni, 2018	1. Jamii kupewa elimu ya kuwatambua na kuwapa huduma za jamii watoto wanaohitaji huduma	Idadi ya watoto wanaoishi kwenye mazingira magumu waliopata huduma za jamii	

IDARA YA AFYA

Tatizo	Dhumuni	Lengo	Mikakati	Viashiria	Mhusika
Upungufu wa dawa na vifaa tiba kwenye Vituo vya kutolea huduma za afya	Kuboresha huduma za afya kwa Wananchi wa Missenyi	Kupunguza ukosefu wa dawa na vifaa tiba kutoka asilimia 40% kufika asilimia 30% ifikapo Juni, 2018	1. Kuhakikisha takwimu sahihi za matumizi ya dawa zinatumika katika uagizaji wa dawa na vifaa tiba	Taarifa zenye takimwu sahihi kwa kila robo	Halmashauri Wenye maduka ya dawa Vituo vinavyotoa huduma
			2. Kuandaa,kuidhinisha na kuhakiki mahitaji ya robo ya dawa na vifaa tiba kupitia ILS	Mahitaji ya kila kituo kwa robo mwaka kupitia ILS	
			3. Kuhakikisha matumizi sahihi ya dawa na vifaa tiba vilivyopo katika vituo vya kutolea huduma za afya yanafuatwa kulingana na taratibu	Takwimu sahihi za matumizi ya dawa na vifaa tiba	
			4. Kuhakikisha makusanyo na matumizi sahihi ya pesa kutoka vyanzo vya ndani vya vituo yanazingitiwa	Kiasi cha fedha kilichokusanywa na Kiasi cha pesa kilichotumika	
			5. Kuhakikisha maduka ya dawa muhimu na Vituo vya kutolea huduma vya watu binafsi vinatoa huduma stahiki kwa jamii	Idadi ya maduka yanayotoa huduma Idadi ya Vituo vinavyotoa huduma	
Uwepo wa magonjwa yanayoathiri jamii.	Jamii ya Missenyi kutokuwa na magonjwa yanayoathiri afya zao	Kupunguza vifo vya watoto walio chini ya miaka 5 kutoka 3/1000 hadi 2/1000 ifikapo Juni 2018	Kushirikisha jamii katika kinga ya magonjwa na namna bora ya kutoa huduma ya kiafya kwa watoto chini ya miaka 5	Taarifa ya kupungua kwa kiwango cha vifo vya watoto.	
		Kupunguza maambukizi ya malaria kwa wagonjwa kutoka asilimia 33 hadi10% ifikapo Juni, 2018	1. Kuhakikisha kinga na matibabu bora kwa wagonjwa wa malaria katika jamii. 2. Kuhakikisha mazalia ya mbu katika jamii yanatokomezwa	✓ Kiwango cha maambukizi kilichopungua ✓ Idadi ya mazalia ya mbu yaliyotokomezwa	Jamii Halmashauri

Kuongezeka kwa maambukizi mapya ya VVU/UKIMWI	Kutokuwa na maambukizi mapya Wilayani	Kupunguza maabukizi mapya ya VVU UKIMWI kutoka 3.4% hadi 3% ifikapo Juni 2018	Kushirikisha jamii katika kupanga na kushiriki katika kutoa elimu ya kubadili tabia	Kiwango cha maambukizi mapya kilichopungua	Jamii Halmashauri NGOs CSOs
		Kuongeza idadi ya vituo vinavyotoa huduma bora za kifua kikuu na ukoma kutoka 9 hadi 16 ifikapo june 2018	1. Kuhakikisha watumishi wote wa afya wana elimu juu ya ugunduzi wa magonjwa ya kifua kikuu na ukoma 2. Kuhakikisha elimu ya tiba sahihi ya Ukoma na Kifua Kikuu imeeleweka miongoni mwa Jamii	Idadi ya vituo vilivyoongezeka Idadi ya watu waliopewa elimu ya tiba sahihi ya Ukoma na Kifua kikuu	
Wazee wa miaka 60 na kuendelea kukosa huduma ya afya bila malipo	Wazee wa miaka 60 na kuendelea kupata huduma ya afya bila malipo	Wazee wenye umri wa miaka 60 na kuendelea wapatao 10,000 kupewa huduma ya afya bila malipo ifikapo Juni 2018	1. Kuhakikisha dirisha la wazee linafunguliwa kwa kila kituo cha kutolewa huduma za afya. 2. Kuendelea kuwatambua wazee wenye miaka 60 katika Wilaya ya Missenyi. 3. Kuwa na bajeti kila mwaka ya kuwasaidia Wazee wa mika 60 na kuendelea	✓ Idadi ya wazee waliotambuliwa na kupewa vitambulisho. ✓ Idadi ya wazee waliopata matibabu bila kulipia ✓ Bajeti inayowasaidia Wazee kupata huduma za afya bila kulipia	✓ Halmashauri ✓ Chama cha Wazee Missenyi ✓ Jamii
Uhaba wa watumishi wa idara ya Afya	Idara ya afya kuwa na watumishi wa kutosha	Kuongeza idadi ya watumishi toka 194 hadi 294 ifikapo june 2018	Kuwa na bajeti ya kuajiri watumishi wapya	Idadi ya watumishi wapya walioajiriwa.	Halmashauri Serikali kuu
Uhaba wa Miundo mbinu ya kutolea huduma bora za afya	Kuwa na miundo mbinu za kutosha za kutolea huduma za afya	1. Kuongeza Vituo vya afya toka 1 hadi 5 na Zahanati 30 hadi 35 na nyumba za Watumishi toka 44 hadi 49 ifikapo Juni, 2018	Kuhamasisha jamii kila Kijiji, NGOs, CSOs na Watu binafsi kushiriki kikamilifu katika ujenzi wa Zahanati, nyumba za Watumishi na Vituo vya afya	Idadi ya vituo vya afya na zahanati vilivyojengwa	Jamii

IDARA YA MAJI

Tatizo	Dhumuni	Lengo	Mikakati	Viashiria	Wadau
Uhaba wa upatikanaji wa maji safi na salama katika jamii	Kuongeza upatikanaji wa huduma za maji kwenye jamii .	Upatikanaji wa huduma ya maji Vijijini kuongezeka toka asilimia 53% hadi 73% ifikapo Juni 2018.	1. Kuunda na kuimarisha jumuiya za watumiaji maji. 2. Miundo mbinu ya maji isiyotoa maji kukarabatiwa 3. Kuwa na Bajeti ya kujenga miundo mbinu ya maji 4. Elimu ya kusimamia na kuendesha miundo mbinu ya maji kutolewa kwa Watumia maji 5. Kusanifu na kuandaa michoro ya miundo mbinu za maji	Idadi ya jumuiya ya Watumia maji zilizoimarishwa Idadi ya miundo mbinu zilizokarabatiwa Bajeti ya Maji Idadi ya Watumia maji waliopata maunzo ya kusimamia na kuendesha miundo mbinu ya maji Idadi ya michoro ya miundo mbinu ya maji iliyoandaliwa	Jamii Wizara ya fedha Halmashauri Vikundi vya Watumia maji DWE
Uhaba wa watumishi kwenye Idara	Kuwa na Watumishi wa Idara wa kutosha	Kuongeza/ kuajiri Watumishi wapya toka 3 hadi 7 ifikapo Juni 2018	1. Kutoa taarifa wizara ya utumishi juu ya uhaba wa watumishi. 2. Kuweka mpango na bajeti ya kuajiri Watumishi wapya.	Idadi ya Watumishi wapya walioajiriwa.	Serikali kuu Halmashauri

IDARA YA ELIMU MSINGI

Tatizo	Dhumuni	Lengo	Mikakati	Viashiria	Mhusika
Kutokamilika kwa ufundishaji wa mihtasari ya masomo kwa shule za msingi.	Uinuaji wa kiwango cha elimu na upatikanaji wa huduma za jamii kuboreshwa.	Ufundishaji wa mihtasari ya masomo kwa shule za msingi kufikia kitabu 1 kwa mwalimu 1 badala ya kitabu 1 kwa walimu 3 ifikapo Juni 2018	1. Kuwa na bajeti kila mwaka ya kununua vitabu vya walimu 2. Kuhamasisha Wadau wa elimu kununua vitabu vya kufundishia	**I**dadi ya vitabu vilivyonunuliwa	Halmashauri Wadau wa elimu Serikali kuu Wakaguzi wa sule Wazazi Walimu
Kiwango cha chini cha ufaulu wa darasa		Kuinua kiwango cha ufaulu wa darasa la VII kutoka 72.22% hadi 90% ifikapo Juni 2018	1. Kuthibiti utoro wa walimu na wanafunzi 2. Kuongeza motisha kwa walimu	Idadi ya wanafunzi watakaofaulu darasa la saba. Kamati za Shule	

Tatizo	Dhumuni	Lengo	Mikakati	Viashiria	Mhusika
la saba			3. Kufanya mitihani ya majaribio kwa kila kata	zinazotekeleza wajibu wao Walimu walioendelezwa/	
			4. Kuwaendeleza walimu kitaaluma 5. Kuimarisha kamati za taaluma kwa kila shule na ngazi ya Kata	watoro waliochukuliwa hatua	
Wanafunzi kutopata stadi za kudumu kusoma, kuandika na kuhesabu (KKK)		Kuinua kiwango cha ufaulu wa darasa la IV kutoka asilimia 90.9 hadi asilimia 96 ifikapo Juni 2018 .	1. Wanafunzi kufanya Mitihani mingi ya majaribio kwa kila Shule, Kata na Wilaya. 2. Kuboresha vituo vya MEMKWA 3. Kuandaa walimu wa kufundisha KKK	Idadi ya wanafunzi watakaofaulu Idadi ya wanafunzi watakaojua KKK Idadi ya Walimu walioandaliwa	
Watoto wenye umri wa kuanza darasa la kwanza kutoandikishwa		Kuongeza kiwango cha uandikishaji kwa madarasa ya awali kutoka 5,920 hadi 6,239 na wanafunzi 6,239 hadi 6,460 kwa Darasa la I ifikapo Juni 2018.	1. Kushirikisha jamii katika zoezi la uandikishaji	Idadi ya watoto walioandikishwa darasa la awali na la I	
		Kuinua kiwango cha taaluma kwa walimu 66 hadi 102 katika ngazi ya stashahada na shahada ifikapo Juni 2018.	Kuwa na mpango wa kuwaendeleza walimu kitaaluma	Idadi ya walimu walioendelezwa	Walimu Serikali kuu Halmashauri
Idadi ndogo ya walimu shuleni.	Kuwa na Walimu wanaotosha kwa uwiano wa wanafunzi kwenye	Kuongeza walimu kutoka 851 hadi walimu1,050 ifikapo Juni 2018	1. Kuwa na bajeti ya kuwaajiri walimu wapya na mbadala	Idadi ya walimu walioajiriwa	Halmashauri Serikali kuu

	Shule zote				
Mazingira magumu ya kufundishia	Kuboresha mazingira		1. Kushirikisha jamii kuchangia ujenzi wa miundo mbinu ya shule	Idadi ya nyumba zilizojengwa Idadi ya walimu wanaoishi kwenye nyumba	Halmashauri
na kujifunzia	mazuri ya kujifunzia na kufundishia	Kuongeza nyumba za walimu kutoka 230 hadi 251 ifikapo Juni 2018	2. Kuwa na bajeti ya kujenga miundo mbinu za shule	Idadi ya vyumba vya madarasa vilivyojengwa	Wadau wa elimu
		Kuongeza vyumba vya madarasa 657 hadi 673 Ifikapo Juni 2018			
		Kuongeza matundu ya vyoo kutoka 1,024 hadi 1140 ifikapo Juni 2018		Idadi ya matundu ya vyoo yaliyojengwa	Wananchi Serikali kuu
		Kuongeza idadi ya madawati kutoka 14,072 hadi 19,072 ifikapo Juni 2018.	Kushirikisha jamii kuchangia utengenezaji wa madawati Kuwa na bajeti ya kutengeneza madawati	Idadi ya madawati yaliyotengenezwa	
		Kuongeza idadi ya vitabu vya ziada na kiada kutoka 94,249 hadi vitabu 99,249 ifikapo Juni 2018	1. Kuwa na bajeti ya kununua vitabu 2. Kuhakikisha vitabu vinagawiwa kwa uwiano	Idadi ya vitabu vilivyonunuliwa	
		Kuongeza idadi ya ofisi za walimu kutoka 189 hadi 200 ifikapo Juni 2018	1. Kushirikisha jamii kuchangia ujenzi wa miundo mbinu za shule 2. Kuwa na bajeti kila mwaka	Idadi ya ofisi za walimu zilizojengwa	
		Kuongeza vituo vya ufundi stadi 2 na kituo cha elimu jumuishi 1 ifikapo Juni 2018.	1. Kushirikisha jamii kuchangia ujenzi wa miundo mbinu ya vyuo 2. Kuwa na bajeti kila mwaka	Idadi ya vituo vya ufundi stadi vilivyojengwa Idadi ya kituo cha elimu jumuishi kilichojengwa	

		Kuongeza shule moja Kijiji cha Bubale Kata Kakunyu na Bunazi ifikapo Juni 2018	1. Kushirikisha Jamii katika uchangiaji ujenzi wa miundo mbinu ya shule	Idadi ya madarasa yaliyojengwa Idadi ya wanafunzi wanaosoma darasani	Wadau wa michezo Vyama vya michezo Jambo Bukoba Wanafunzi Walimu Halmashauri Baraza la Michezo (W/M)
		Kuhakikisha upatikanaji wa huduma ya chakula/uji katika shule 78 kati 102 kufikia Juni 2018	1. Jamii kushirikishwa kuchangia uji/chakula 2. Kuazisha na kuendeleza elimu ya kujitegemea shuleni.	Idadi ya shule zinazotoa uji/chakula Idadi ya vifaa vya EK.	
Kutokuwa na ukakamavu shuleni na Vijana wengi nje ya shule kutoshiriki michezo	Kuinua vipaji na kuimarisha ukakamavu kwa wanafunzi Shuleni	Kushiriki UMITASHUMTA kila mwaka ifikapo Juni, 2018		Idadi ya vilabu vilivyoanzishwa. Timu za shule bora na zenye ushindani	
			1. Kuhamasisha kila kata kuanzisha na kusajili vilabu vya mpira 2. Kuwa na timu imara za kila shule		Chama cha Wazee Missenyi Kata na Vijiji
		Kupima viwanja 18 vya michezo kati ya 100 vilivyopo kwenye shule	1.Kuainisha shule zenye maeneo ya viwanja 2. Kuandaa kamati za michezo za kuratibu upimaji	Idadi ya viwanja vilivyopimwa.	
		Kuongeza vyama vya michezo 3 kutoka kimoja ifikapo JunI 2018.	1. Kupokea miongozo na kusajili vyama.	Idadi ya vyama vya michezo vilivyoanzishwa.	

Kumbukumbu za Mila na Tamaduni za Kiaya kutopewa kipaumbele	Kuwa na makumbusho ya mila na tamaduni za Kihaya	Kuboresha kumbukumbu za mila na tamaduni za Kihaya 4 kati ya 5 zilizopo ifikapo Juni 2018	1. Kuhamasisha jamii kupitia serikali za mitaa ili kutambua na kuboresha maeneo ya kumbukumbu za Mila na Tamaduni za Kihaya. 2. Kushirikisha Wazee katika kutambua na kuenzi mila na tamaduni	Idadi ya maeneo aliyotambuliwa na kuhifadhiwa	

IDARA YA ELIMU SEKONDARI

Tatizo	Dhumuni	Lengo	Mikakati	Viashiria	Mhusika
Upungufu wa shule za Sekondari za kidato I hadi kidato IV ndani ya Wilaya	Kuwa na shule za Sekondari katika Kata zenye idadi kubwa ya wanafunzi	1. Shule za Sekondari kuongezeka toka 27 hadi shule 31 ifikapo Juni, 2018	1.Kutambua Kata zenye idadi kubwa ya wanafunzi wanaojiunga kidato cha I kila mwaka 2.Kuwashirikisha wadau wa elimu katika kuongeza miundombinu	Idadi ya Kata zilizotambuliwa	World Vision Wadau wa Elimu
Upungufu wa shule za Sekondari za kidato V hadi kidato VI ndani ya Wilaya	Kuwa na shule za Sekondari za kidato cha V na VI katika kila Tarafa	2. Shule za sekondari za serikali zenye kidato cha V na VI kuongezeka toka 1 hadi 2 ifikapo Juni, 2018	1.Kuwashirikisha wadau wa elimu na Wananchi katika kujenga miundombinu ya Sekondari ya kidato cha V na VI	Idadi ya shule ya kidato cha V na VI iliyojengwa	Halmashauri Jamii
Mazingira magumu ya kufundishia na kujifunzia	Kuwa na muindombinu ya kutosha kila shule za Sekondari	3. Vyumba vya madarasa kuongezeka toka 220 hadi 328 ifikapo Juni, 2018	1.Kutambua shule zenye upungufu wa vyumba vya madarasa katika shule 27 za sekondari 2 Kuwashirikisha wadau wa elimu katika kuongeza vyumba vya madarasa katika Wilaya.	Idadi ya shule zilizotambuliwa. Idadi ya miundombinu zilizojengwa	Serikali kuu MAPEC

		4. Nyumba za walimu kuongezeka toka 37 hadi 91 ifikapo Juni, 2018 5. Matundu ya vyoo kuongezeka toka matundu ya vyoo 311 hadi 419 ifikapo Juni, 2018	1.Kutambua shule zenye upungufu wa nyumba za Walimu na matundu ya vyoo kwenye shule 27 Kuwashirikisha wadau wa elimu katika kuongeza matundu ya vyoo katika shule za sekondari	Idadi ya nyumba zilizojengwa Idadi ya matundu ya vyoo yaliyojengwa	TADEPA Kagera Sugar
		Maktaba kuongezeka toka 8 hadi 27 ifikapo Juni, 2018	1. Kutambua shule zenye upungufu wa maktaba na ofisi za walimu katika shule 27 za sekondari 2. Kuwashirikisha wadau wa elimu katika kuongeza maktaba katika shule za sekondari	Idadi ya shule zenye mapungufu ya maktaba Idadi ya maktaba zilizojengwa	Halmashauri
		Ofisi za walimu kuongezeka toka ofisi 19 hadi 27 ifikapo Juni, 2018		Idadi ya shule zenye upungufu wa ofisi za walimu Idadi ya ofisi za walimu zilizojengwa	Wadau wa Elimu
		Maabara kuongezeka toka maabara 30 hadi maabara 81 ifikapo Juni, 2018	1.Kutambua shule zenye upungufu wa maabara katika shule 27 za Sekondari 2 Kuwashirikisha wadau wa elimu katika kuongeza maabara kwenye shule za Sekondari	Idadi ya shule zenye upungufu wa maabara Idadi ya maabara zilizojengwa	Serikali Jamii
		Stoo za kutunzia vifaa/mali za shule kuongezeka toka stoo 9 hadi stoo 27 ifikapo Juni, 2018	1.Kutambua shule zenye upungufu wa stoo katika shule 27 za Sekondari 2. Kuwashirikisha wadau wa elimu kujenga stoo za walimu katika shule za sekondari	Idadi ya shule zenye upungufu wa stoo Idadi ya stoo zilizojengwa	
Upungufu wa watumishi/walimu	Kuwa na walimu wa kutosha na kwa uwiano	Walimu kuongezeka toka walimu 333 hadi walimu 471 ifikapo Juni, 2018	1.Kutambua mahitaji ya walimu kwa uwiano wa wanafunzi na mwalimu 2. Kuwa na bajeti ya kuajiri kila	Idadi ya walimu walioajiriwa Uwiano wa	Serikali Halmashauri Jamii

	wa wanafunzi kwenye shule za Sekondari		mwaka	Wanafunzi na mwalimu kitaifa	Idara ya Ukaguzi
Kiwango cha chini cha ufaulu	Ubora wa elimu ya Sekondari kuongezeka	Kiwango cha ufaulu kidato IV kupanda toka aslimia 35% hadi 45% ifikapo Juni, 2018	1. Ufundishaji kwenye shule za sekondari 27 kuimarishwa	Idadi ya shule zilizokaguliwa Kiwango cha ufaulu	Wanafunzi Walimu Wazazi Halmashauri Serikali kuu
		1. Kiwango cha ufaulu kidato II kuongezeka toka 30% hadi 51% ifikapo Juni, 2018 2. Kiwango cha ufaulu kidato VI kuongezeka na kufikia 85% ifikapo Juni, 2018	1. Kuimarisha ufundishaji kwenye shule za sekondari 27	Kiwango cha ufaulu wa kidato cha VI	

IDARA YA USAFI NA MAZINGIRA

Tatizo	Dhumuni	Lengo	Mikakati	Viashiria	MHUSIKA
Uchafuzi wa mazingira katika jamii	Kupunguza magonjwa yasababishwayo na uchafuzi wa mazingira.	Kuinua kiwango cha usafi wa mazingira kutoka 37% za sasa hadi 57% ifikapo Juni, 2018.	Kushirikisha jamii kutambua umuhimu wa usafi wa mazingira na madhara yake	Kupungua kwa magonjwa yanayotokana na uchafuzi wa mazingira .	Wananchi Halmashauri Wadau wa mazingira
			Kuhakikisha sheria ndogo za usafi wa mazingira zinafanya kazi.	Idadi ya watu waliochukuliwa hatua za kisheria.	Halmashauri Wananchi WEOs/VEOs
Uhaba wa watumishi katika idara	Kuwa na Watumishi wa kutosha	Kuongeza watumishi toka 1 hadi 5 ifikapo Juni 2018.	Kutoa taarifa Serikali kuu kuhusu uhaba wa watumishi	Idadi ya watumishi wanaotakiwa	Halmshauri Serikali kuu
			Kuweka katika mpango na kutenga bajeti ya watumishi wapya.	Bajeti ya watumishi wapya kuonekana katika mpango	Halmashauri

IDARA YA UTAWALA

Tatizo	Dhumuni	Lengo	Mikakati	Viashiria	Mhusika
Huduma isiyo na ubora kwa jamii	Kutoa huduma bora kwa jamii	Idadi ya Watumishi wa Kada mbali mbali kwenye Halmashauri kuongezeka toka watumishi 2,146 hadi Watumishi 3,200 ifikapo Juni, 2018	1. Kuomba vibali vya ajira 2. Kuimarisha mazingira bora ya kufanyia kazi	Idadi ya Wananchi waliopata huduma bora Idadi ya watumishi waloajiriwa	Halmashauri
Mazingira yasiyoridhisha ya kufanyia kazi	Kuboresha mazingira ya kufanyia kazi	Nyumba za watumishi kuongezeka toka nyumba 8 za sasa hadi nyumba 20 ifikapo Juni, 2018	Kuhamasisha Taasisi zingine kujenga nyumba za kuishi kwenye miji ya Bunazi , Mutukula na Kyaka	Idadi ya nyumba za watumishi zilizojengwa Mutukula, Kyaka na Bunazi	Watumishi Serikali kuu
		Ofisi za Kata kuongezeka toka 4 hadi 14 ifikapo Juni, 2018	Kuishirikisha jamii kujenga ofisi za Kata na Vijiji	Idadi ya ofisi zitakazojengwa. Idadi ya Wananchi wanaopata huduma bora	
		Ofisi za Vijiji kuongezeka toka 8 hadi 18 ifikapo Juni, 2018		Idadi ya ofisi zitakazo jengwa. Huduma itakayotolewa	
Utendaji kazi usiyoridhisha	Kuboresha utendaji kazi	Ujuzi na Ueledi wa kazi kwa Watumishi kuongezeka kwa Watumishi 200 kwenye Idara na Vitengo ifikapo Juni 2018	Kuwaruhusu watumishi kujiendeleza Watumishi wanaojituma na Wabunifu kuzawadiwa	Idadi ya watumishi waliojiendeleza Kiwango cha utendaji kazi Watumishi waliozawadiwa	
		Samani za ofisi kuu, Kata na Vijiji kuongezeka toka 50% hadi 90% ifikapo Juni, 2018	Kuwa na uwiano mzuri wa samani na watumishi	Idadi ya samani ofisini Watumishi kukaa ofisini	Halmashauri Wakuu wa idara Watumishi
Malalamiko ya watumishi kupata stahili	Kuhuisha taarifa za watumishi	Kuboresha taarifa za watumishi kutoka 70% hadi 98% ifikapo Juni 2018	Kuhuisha taarifa za watumishi Kuwajulisha	% ya malalamiko ya watumishi Taarifa za watumishi	Halmashauri

zao			watumishi wenye mapungu kwenye taarifa zao		
Kukwama kwa shughuli za maendeleo	Demokrasia ushiriki wa jamii kuimarika katika shughuli za maendeleo	Kuongeza kiwango cha ushirikishwaji wa wananchi katika kutoa maamuzi kutoka 67% za sasa hadi 90% ifiapo Juni 2018	Kuhakikisha jamii ina hamasika katika shughuli za maendeleo Kushirikisha jamii katika kutoa maamuzi	% za shughuli za maendeleo vijijini	Afisa Utumishi Afisa Mipango WEOs & VEOs Jamii
Ushiriki mdogo wa jamii katika kutekeleza utawala bora na kupambana na Rushwa	Demokrasia na ushiriki wa jamii kuimarika katika shughuli za maendeleo	Kuongeza kiwango cha ufanyikaji wa mikutano yote ya kisheria ngazi ya Vijiji na Vitongoji kutoka 60% hadi 90% ifikapo Juni, 2018	Kuhakikisha jamii ina hamasika katika kuhudhuria mikutano Kushirikisha jamii katika kutoa maamuzi	Idadi ya vikao na mikutano inayofanyika	WEOs VEOs Jamii Wahe. Wenyeviti wa WDC/VCs/ Vitongoji
			Kuhakikisha wananchi wanaelimishwa juu ya madhara ya kutoa au kupokea rushwa	Idadi ya Wananchi waliopata mafunzo ya madhara ya rushwa	TAKUKURU Jamii Viongozo ngazi zote
Huduma ya usafirishaji isiyoridhisha	Kuboresha huduma ya usafirishaji	Kuimarisha huduma ya Usafiri na usafirishaji kutoka 50% ya sasa hadi 80% iikapo Juni, 2018	Kuwa na bajeti ya kununua magari mapya na ya matengenezo ya magari	Idadi ya magari yanayotembea Mapato yotokanayo na magari ya kukodishwa	Halmashauri
Waheshimiwa Madiwani kutokuwa na uzoefu wa kutosha kuongoza Halmashauri	Waheshimiwa wanaochaguliwa kuwa na uzoefu wa kuendesha Halmashauri	Waheshimiwa wote watawezeshwa kupata uzoefu wa kuendesha Halmashauri mara baada ya Uchaguzi Mkuu 2015 ifikapo Juni, 2018	Kuhudhuria semina, mafunzo na kufanya zira ya mafunzo	Idadi ya Wahe. Watakaopata mafunzo	Halmashauri Serikali kuu Wahe. Madiwani
Ongezeko la migogoro	Kuwa na Jamii isiyo na	Kupunguza migogoro na mfarakano baina ya Jamii	1. Wanajamii kutambua haki zao	Idadi ya migogoro iliyosuluhishwa	Jamii Halmashauri

kwenye jamii.	migogoro na mfarakano baina yao	toka asilimia 45 hadi 59 ifikapo Juni, 2018	2. Kuhakikisha haki za jamii zinalindwa, hasa Wanawake, Watoto na Makundi maalum	Idadi ya jamii iliyolindwa	

IDARA YA MIPANGO

Tatizo	Dhumuni	Lengo	Mikakakti	Viashiria	Muhusika
Ushiriki mdogo wa jamii katika kupanga, kutekeleza, kufuatilia na kutathimini miradi ya maendeleo.	Demokrasia,Ushiriki wa Jamii na Utawala Bora kuimarika	Kuimarisha mfumo shirikishi wa upangaji, utekelezaji, ufuatiliaji na tathimini ya miradi ya maendeleo toka 70% hadi 80% ifikapo juni 2018	1. Kuhakikisha jamii inashiriki katika kuibua, kupanga, kutekeleza, kufuatilia na kutathimini miradi ya maendeleo. 2. Kuhakikisha Uwekezaji kwenye nyanja zote za kiuchumi, kiutamaduni na kijamii	Idadi ya Watu wanaoshiriki kwenye miradi ya maendeleo Mradi iliyokamilika na kutoa huduma. Vikao vya maamuzi.	Halmashauri Jamii, NGO, WDCs, VCs Wawekezaji
Wilaya kutokuwa na takwimu sahihi za kiuchumi na kijamii	Takwimu mbali mbali kuwepo na kutumiwa kwenye maamuzi	Mfumo wa kukusanya takwimu za kijamii na kiuchumi (LGMD) kuimarishwa toka asilimia 50 hadi 70 ifikapo Juni, 2018	Kuhakikisha Vijiji, Kata, Halmashauri na Wadau wote wanakusanya na kutunza takwimu mbali mbali	Idadi ya takwimu sahihi zilizokusanywa	Wadau Halmashauri WEOs VEOs
Miradi mingi kutofuatiliwa na kutathminiwa	Kuwa na ufuatiliaji na tathmini ya miradi inayotekelezwa Wilayani	Mfumo wa ufuatiliaji na tathmini kuimarishwa toka asilimia 60 hadi 80 ifikapo Juni, 2018	1. Kuhakikisha Wadau wote wanashirikishwa kwenye mchakato wa ufuatiliaji na tathmini ya miradi inayotekelezwa 2. Kushirikisha Wadau wa maendeleo kwenye tathmini ya pamoja ya shughuli za maendeleo ya Halamshauri	Idadi ya Wadau wanaoshiriki kwenye ufuatiliaji Idadi ya Wadau wanaoshiriki kwenye tathmini Idadi ya mikutano ya tathmini	Wadau wote wa maendeleo Halmashauri

IDARA YA FEDHA NA BIASHARA

Tatizo	Dhumuni	Lengo	Mikakati	Viashiria	Mhusika
Kiwango kidogo cha uwajibikaji katika kukusanya mapato.	Halmashauri kuwa na uwezo kifedha kuwahudumia Wananchi kiuchumi na kijamii	Kiwango cha ukusanyaji wa mapato kuongezeka toka 1,090,000,000 hadi 1,395,200,000 ifikapo Juni, 2018.	1. Kuhakikisha uwepo wa uhalisia wa takwimu za vyanzo vyote vya mapato 2. Kuwashirikisha jamii na Wadau kukusanya mapato ya ndani 3. Kuhakikisha taratibu zinazotumika kukusanya mapato zinaimarishwa 4. Kuhakikisha viwango vya mapato vinarejelewa kila mara kwa lengo la kuongeza pale inapobidi. 5. Elimu ya umuhimu wa kutoa ushuru na kodi kwenye Halmashauri kutolewa kwa Jamii na Wadau	Takwimu za vyanzo vya mapato zilizokusanywa. Asilimia ya kiwango cha ushiriki wa jamii katika kutoa mapato. Sheria ndogondogo zilizohuishwa na taratibu za ukusanyaji. Viwango vya mapato vilivyorekebishwa Idadi ya Jamii na Wadau waliopata elimu ya umuhimu wa kutoa kodi na ushuru	Halmashauri Wadau wa mapato Viongozi ngazi zote WEOs, VEOs Jamii
Kutokuwa na vyanzo vya mapato ya ndani vyente uhakika		Vyanzo vya mapato vinavyoaminika kuongezeka toka 10 hadi 20 ifikapo Juni, 2018	Kuwezesha uwekezaji kwenye sekta za: Biashara, Kilimo, Mifugo na Viwanda	Idadi ya vyanzo vya mapato vya uhakikka vilivyoanzishwa Idadi ya Viwanda vilivyoanzishwa	Wawekezaji Halmashauri
Uhaba wa watumishi		Idadi ya Watumishi kuongezeka toka 11 hadi 19 ifikapo Juni, 2018.	Kuwa na bajeti ya kuajiri Watumishi wapya/mbadala .	Idadi ya Watumishi walioajiriwa	Halmashauri Serikali kuu
Kutokuwa na umakini wa kufuata taratibu, kanuni na sheria za Fedha	Sheria, Kanuni na taratibu za matumizi ya fedha za Serikali za Mitaa kufuatwa	Kupunguza hoja za ukaguzi toka asilimia 30 hadi 10 ifikapo Juni, 2018	1. Wakuu wa Idara na Vitengo na Watoa huduma kupata elimu ya taratibu za fedha 2. Hoja za ukaguzi kupata majibu mapema 3. Kumbukumbu na taarifa	Idadi ya Wakuu wa Idara/Vitengo na Wadau waliopata elimu Idadi ya hoja zilizojibiwa Idadi ya ya Hati safi iliyopatikana	Halmashauri Wadau

			za fedha kutunzwa vizuri		

KITENGO CHA SHERIA

Tatizo	Dhumuni	Lengo	Mikakati	Viashiria	Muhusika
Jamii kutojua haki zao za msingi	Demokrasia na Utawala Bora kuimarika miongoni mwa Jamii	Demokrasia na Utawala bora kuimarishwa toka asilimia 50 hadi 80 ifikapo Juni 2018	1.Jamii kuelewa dhana ya utawala bora na utawala wa sheria kwa vitendo 2.Sheria mbali mbali za: Nchi, Halmashauri, na Vijiji kueleweka kwa Jamii 3.Kuimarisha huduma ya msaada wa kisheria kwa Jamii	Idadi ya watu wanaofahamu sheria Sheria ndogo za Halmashauri na vijiji zilizotungwa. Idadi ya watu waliopata huduma za kisheria	Jamii Halmashauri Mahakama NGOs Para Legal Systems

KITENGO CHA TEHAMA

Tatizo	Dhumuni	Lengo	Mikakati	Viashiria	Mhusika
Ukosefu wa huduma ya uhakika ya mtandao kwenye jengo la Halmashauri	Halmashauri kuwa na mawasiliano mazuri na Taasisi zingine za ndani na nje	1. Kuwa na ***Tovuti*** ya Halmashauri ifikapo Juni, 2018 2. Kuwa na Mtandao wa ***'Internet'*** kwenye jengo la Halmashauri ifikapo Juni, 2018	1. Kuwa na bajeti ya kuweka Tovuti ya Halmashaurina mfumo wa 'Internet' 2. Kuwashirikisha Wadau kutoa taarifa na takwimu mbali mbali za kiuchumi, kijamii, kiutamaduni na kisiasa Wilayani na Mkoani	Tovuti iliyoanzishwa Mtandao wa Internet iliyowekwa kwenye jengo la Halmashauri	Halmashauri TTCL Wadau

KITENGO CHA UCHAGUZI

Tatizo	Dhumuni	Lengo	Mikakati	Viashairia	Mhusika
Ushiriki mdogo wa Wananchi kwenye shughuli za Siasa	Wananchi kushiriki kwenye shughuli za Siasa kwa njia ya Demokrasia na kwa amani	Kuimarisha demokrasia miongoni mwa Jamii na Vyama vya Siasa toka asilimia 60% hadi 80% ifikapo Juni, 2018	1. Elimu ya demokrasia kutolewa kwa Jamii na Viongozi wa Vyama vya Siasa Wilayni 2. Kuwa na Chaguzi zinazofanyika kwa huru na haki 3. Elimu ya upigaji kura kutolewa kwa Jamii na Viongozi wa VCyama vya Siasa	Idadi ya Jamii na Viongozi wa vyama vya Siasa waliopata elim Idadi ya chaguzi zilizofanyika kwa huru na haki	Vyama vya siasa Jamii Halmashauri Wanaharakati NGOs/CBOs

KITENGO CHA UKAGUZI WA NDANI

Tatizo	Dhumuni	Lengo	Mikakati	Viashairia	Mhusika
Ukiukaji wa taratibu, kanuni na sheria za fedha)	Taratibu, Kanuni na Sheria za fedha za Serikali za Mitaa (LAFM na LAFA) kuzingatiwa muda wote	Kuimarisha shuguli za ukaguzi wa mahesabu toka asilimia 70 hadi 90 ifikapo Juni, 2018	1. Kuhakikisha Wada wote wana uelewa wa pamoja kuhusu taratibu, kanuni na shareia ya fedha za Serikali za Mitaa 2. Kuhakikisha Wadau wote wanapata elimu ya sheria na kanuni za manunuzi 3. Kuhakikisha Wadau wote wanatunza kumbukumbu zote za fedha	Idadi ya Wadau waliopata elimu ya sheria za fedha na Manunuzi Idadi ya kumbukumbu za fedha zilizotunzwa	Wadau Halmashauri VEOs WEOs

SURA YA V

MPANGO KAZI WA KUTEKELEZA MPANGO MKAKATI

5.0 Utangulizi

Mafanikio ya utekelezaji wa MM ndani ya muda wa miaka 5 hutegemea zaidi; Ushirikishwaji wa Jamii, Mpango kazi, Rasilimali fedha, Nyenzo na Vitendea kazi pamoja Wataalamu wa kutosha wenye moyo wa kazi.

Muda wa utekelezaji wa MM ni muhimu sana kwani vipaumbele vya Jamii vinatofautiana kwa kiwango cha madhara au kiasi cha manufaa yanayotakiwa kwa wakati huo. Utekelezaji usioendana na matarajio ya wengi kwa wakati muafaka unaweza kutumia muda na rasilimali fedha bila ufanisi wala tija.

5.1.0 Mpango kazi wa kutekeleza MM

Kila Halmashauri kupitia mpango na bajeti ya kila mwaka, huwa inapanga utekelezaji wake kwa kufuata vipaumbele yaliyomo ndani ya MM wa miaka 5.

Ushirikishwaji wa Jamii, Mpango kazi unaotekelezeka, Uwepo/na matumizi mazuri ya rasilimali fedha, nyenzo na vitendea kazi pamoja na Uwepo wa Wataalamu wa kutosha wenye moyo ni siri kubwa ya mafanikio katika kutekeleza MM kwa kila mwaka.

5.1.1 Ushirikishwaji wa Jamii

Wadau wa kwanza na muhimu wakati wa kutekeleza MM ni wananchi ambao wanaguswa moja kwa moja na madhara ya kutofanikiwa au matunda ya mafaniio ya utekelezaji wa mpango mkakati huo.

Wananchi hao wanapaswa kushirikishwa kwenye hatua zote za utekelezaji; yaani kupanga, kutekeleza, kusimamia na kufanya tathmini ili kupima mafanikio kwa kila mwaka. Wananchi hawana budi kujua mahitaji muhimu anayohitajika, kiasi kilichopo na kile kinachopungua kabla ya kutambua mapungufu hayo yatafidiwa na nani. Kwa maneno mengine, Wananchi kwanza, Serikali na Wadau wengine wa maendeleo baadaye

5.1.2 Mpango kazi

Umahiri wa kuandaa na kutekeleza mpango kazi unaozingatia upatikanaji wa rasilimali watu, rasilimali vitu na rasilimali fedha ni kiashiria tosha cha mafanikio ya utekelezaji wa MM. Pale inapobidi, mpango kazi unapaswa kuandaliwa kwa kuzingatia mazingira na mabadiliko yanyotokana na hali ya hewa.

Kazi ya ujenzi wa nyumba au barabara hauwezi kupangwa ifanyike wakati wa masika au wakati wa mafuriko, au wakati unaojulikana kuwa vifaa vya ujenzi havipo au wakati magari ya kusoma vifusi, saruji na nondo hayapo.

Aidha, mpango kazi mahiri lazima ioneshe muda wa utekelezaji na mhusika na mwajibikaji mkuu katika utekelezaji huo.

5.1.3 Uwepo wa rasilimali fedha na vitendea kazi

Utekelezaji wa MM unaweza kukwama kama hakuna fedha wala nyenzo na vitendea kazi vinavyohitajika kwa wakati huo, hata kama kuna mpango kazi unaotekelezeka na wananchi wamehamasishwa na wako tayari kutekeleza MM huo.

Halmashauri inatakiwa iangalie uwezo wake kifedha na upatikanaji wa nyenzo na vitendea kazi ili kuwezesha utekelezaji unaotoa matunda tarajiwa baada ya muda uliopangwa. Pale ambapo rasilimali fedha, nyenzo na vitendea kazi havitoshi, ni budi kipaumbele kitekelezwe kwa kuzingatia uwezo kifedha na upatikanaji wa nyenzo na vitendea kazi. Kinyume chake, fedha kidogo na vitendea kazi vichache vinaweza kuelekezwa kutekeleza mradi unaohitaji fedha nyingi na hatimaye mradi huo usikamilishwe kwa wakati huku wananchi wakibaki na kiu yao ya maendeleo au kero. Hii inaweza kuwakatisha tamaa wananchi huku wakikataa kuendelea kuchangia au kuanza kuwatuhumu Viongozi na Watendaji wa ngazi mbaii mbali kwa uzembe au ubadhirifu

5.1.4 Uwepo wa wataalamu wa kutosha na wanaowajibika

Watu ni rasilimali muhimu sana ya kufanikisha utekelezaji wa MM kwani watu ndiyo wanaoweza kutumia rasilimali zote zilizopo kuleta maendeleo ndani ya Jamii. Binadamu huchanganya saruji, maji na mchanga kuwa tofali na hutumia tofali kujenga nyumba ya ukubwa na urefu wo wote.

Kuwepo kwa watu ni kitu kimoja na kutosha kwao kutekeleza jambo kwa ufanisi ni kitu cha pili ambacho ni muhimu sana kwa maendeleo ya Jamii. Ili watekeleze jambo kwa ufanisi na tija, watu wanatakiwa wawe na sifa ya kutekeleza jambo hilo na wawe na moyo wa kulitekeleza

Hivyo, Halmashauri inapaswa kuwa na wataalamu wa kutosha wenye ujuzi, wenye moyo na wanaowajibika kutekeleza MM kwa wakati kama ilivyoainishwa kwenye mpango kazi.

SURA YA VI

UFUATILIAJI NA TATHMINI

6.0 Muda wa Ufuatiliaji na tathmini

Sura hii ya MM inatoa mwelekeo wa namna utekelezaji wa shughuli zilizopangwa kutekeleza MM na hatimaye kufanya tathmini ya muda wa kati na mwisho wa muda wa utekelezaji. Wakuu wa Idara na Vitengo, Wananchi, Viongozi wa ngazi zote za utekelezaji na Wadau wa Maendeleo waliomo ndani na nje ya Wilaya ndiyo wanaotengeneza ushirika huu muhimu. Baada ya kufuatilia utekelezaji kwa karibu, Wadau hawa kwa pamoja hupata nafasi ya kukaa pamoja na kufanya tathmini

Tathmini ya muda wa kati inaruhusu kufanya mabadiliko ya utendaji ndani ya muda wa MM kwa kuzingatia; Changamoto na matatizo yaliyopo pamoja na yale yanayotarajiwa siku za usoni Tathmini hufanyika kila Robo mwaka, Nusu mwaka na baada ya mwaka.

Tathmini ya mwisho wa utekelezaji wa MM (baada ya miaka 5) inatoa nafasi ya kujua kwa undani vikwazo, changamoto na matatizo yaliyosababisha malengo kutofikiwa na hatimaye kufanya marekebisho wakati wa kuandaa MM kwa miaka mingine 5 ijayo.

6.1 Changamoto wakati wa utekelezaji

Halmashauri inaweza kukabiliana na changamoto mbali mali wakati wa utekelezaji na hatimaye kutofanikiwa kwenye malengo yake kwa kiasi kinachotarajiwa.

Baadhi ya changamoto hizi ni:

- ***Kupanda kwa bei ya vifaa:*** Ongezeko la bei ya vifaa kama vile; Vifaa vya ujenzi, mafuta na vilainishi hupelekea gharama za miradi kuwa kubwa na pengine kupunguza ukubwa wa utekelezaji au kukwamisha kabisa uekelezaji .
- ***Utashi wa kisiasa:*** Endapo Wanasiasa hawana mtazamo chanya na utekelezaji wa Mpango Mkakati huu, ni wazi kuwa hawatawahamasisha Wananchi kushiriki kwenye utekelezaji mradi, hasa pale michango ya Wananchi itakapohitajika kwenye utekelezaji. Kama mradi ulipangwa kuwa na sehemu ya Wananchi kuchangia na hawakuchangia, utekelezaji utafikia asilimia chini ya 100
- ***Kuingilia utendaji:*** Hili nalo ni changamoto linaloikabili Halmashauri wakati wa utekelezaji pale ambapo Wanasiasa wanaingilia utekelezaji wa maamuzi halali ya Wananchi na Wataalamu kwa visingizio vya kuwasumbua Wapiga kura
- ***Wadau kuwa na MM tofauti na wa Halmashauri:*** Wadau wa maendeleo kwenye Halmashauri wanapokuwa na MM au Malengo tofauti na yale ya Halmashauri utekelezaji wa pamoja unakosekana kwa vile kila Mdau au Halmashauri hukimbilia kutekeleza aliyoyapanga na si vinginevyo
- ***Ubovu wa Miundombinu ya barabara:*** Utoaji wa huduma bora na kwa wakati hutegemea zaidi ubora wa miundombinu ya barabara kwenye Halmashauri husika. Barabara zisizopitika muda wote ni kikwazo katika kutekeleza MM na pengine kusababisha maeneo mengine kutotekeleza MM kabisa.
- ***Mabadiliko ya hali ya hewa:*** Kwa kiwango kikubwa bado Wakulima wengi nchini hutegemea hali nzuri ya hewa ili kuweza kulima na kuvuna mazao yao, ama kwa chakula au kwa chakula na biashara. Endapo hali ya hewa inabadilika ghafla, matarajio ya Wakulima nayo hubadilika. Pale ukame au mafuriko yanapotokea, Wakulima hukosa mavuno na hatimaye kuwa na njaa sehemu hiyo..

- ***Idadi ndogo ya Wataalamu:*** Utekelezaji wa MM na utoaji wa huduma za kijamii na za kiuchumi unategemea zaidi uwepo wa Wataalamu wa kutosha kwenye Halmshauri. Kinyume na hapo hakuna matarajio makubwa yatakayopatikana.
- ***Ucheleweshaji wa maamuzi:*** Maamuzi ya uhakika unaochukuliwa kwa wakati ndiyo siri ya mafanikio. Kuchelewesha maaumuzi ni kuchelewesha utekelezaji, hasa pale utekelezaji huo ungeweza kukinga hatari au kuleta ufanisi na mafanikio ya kazi.
- ***Magonjwa ya milipuko na Maafa***: Juhudi za makusudi zinatakiwa kuchukuliwa na Mamlaka ya Halmashauri ili kudhibiti magonjwa ya milipuko pamoja na Maafa na Majanga yanayotokea nje ya matarajio ya Binadamu. Pasipo kudhibiti yote haya, kunakuwa na ugumu wa kutekeleza MM kwa mafanikio, kwani fedha nyingi zilizotengwa kutekeleza MM zitaelekezwa kukabiliana na Magonjwa pamoja na madhara yatokanayo na Maafa au Majanga

Halmashauri inatakiwa ijipange katika kukabiliana na changamoto hizi na kuhakikisha kuwa; Ama changamoto hizi na zingine hazitokei wakati wote wa utekelezaji, Au pale zinapotokea Halmashauri inazuia zisilete madhara kwenye utekelezaji kwa nia ya kufanikisha malengo yaliyoainishwa kwenye Mpango Mkakati.

Mpango Mkakati huu utafanyiwa marejeo na tathmini baada ya miaka 5 ya utekelezaji kwa nia ya kuandaa nyingine itakayotekelezwa kwa miaka 5 ijayo; yaani 2019 - 2023